# Nipashe

Jumanne Aprili 27, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580563

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Usajili** VICOBA mwisho Ijumaa



UKURASA 3

**Mtoto** miaka mitano anayedaiwa kubakwa na babu aomba msaada

UKURASA 18


Nipashe TESA
Jumanne Aprili 27, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
ILO inavyokomesha unyanyasaji, ukatili
Udhalifu huu ungetazamwa mimba shuleni zingepungua
Ajabu Watanzania kuishi kinadharia
ELIMU
NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR
WADHALILISHAJI WAMEKOMA
160 waburuzwa kortini

UKURASA 11

# Mpango: Sitamvumilia atakayechezea Muungano

• **Abainisha** changamoto zilizopatiwa ufumbuzi... *Endelea ukurasa 2*





Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kushoto), akifungua kongamano la miaka 57 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

## YALIYOMO

UKURASA WA 5
**NMB YATENGA BIL. 5/- MIKOPO YA BODABODA**

## Waziri awasweka ndani mkurugenzi, mameneja Maji

UKURASA 2



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, akizindua mkopo wa NMB Mastaboda wakati wa hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna na Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki hiyo, Filbert Mponzi (wa pili kushoto) na kushoto ni Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Pikipiki Dar es Salaam, Michael Massawe.

## H/shauri zenye hati chafu mikononi mwa TAKUKURU

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YAITISHA DODOMA JIJI FC** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Rahma Kassim Ali (kulia), akijadiliana jambo na mwanasiasa mkongwe nchini, Getrude Mongella, walipokutana kwenye Kongamano la 57 la Muungano wa Tanzania na Zanzibar lililofanyika ukumbi wa mikutano wa Chimwaga, jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango: Sitamvumilia atakayechezea Muungano

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema katika kipindi chake cha uongozi hatamvumilia mtu yeyote atakayejaribu kuchezea Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alitoa kauli hiyo jana mjini hapa wakati akifungua Kongamano la Miaka 57 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, lililowashirikisha mawaziri, makatibu wakuu, wabunge, vyama vya siasa, viongozi wa dini na wanafunzi kutoka taasisi za elimu ya juu.

Kaulimbiu ya Miaka 57 ya Muungano kwa mwaka huu inasema "Muungano wetu ni msingi imara wa mapinduzi ya kiuchumi, tudumishe mshikamano".

Akifungua kongamano hilo, Dk. Mpango alisema: "Katika hili nikiwa kama Makamu wa Rais sitakubali kuona mtu anachezea Muungano wetu. Kuna baadhi ya mambo watu walikuwa wanasema kwamba mimi ni mpole, nataka kuwaambia kwamba sitamvumilia mtu na wataona ukali wangu."Kadhalika, Dk. Mpango alisema changamoto 15 kati ya 25 zilizokuwapo katika muungano zimetatuliwa na zilizobakia zinaendelea kutatuliwa.

Vilevile, alisema katika kipindi cha miaka 57 kumepatikana mafanikio lukuki, kutoa rai kwa pande mbili za Muungano kutobeza mafanikio hayo.

Dk. Mpango alitaja baadhi ya mafanikio hayo kuwa ni kuimarika kwa undugu wa damu kwa wananchi wa pande zote mbili, kudumu kwa umoja na mshikamano.

Nyingine ni kuimarika kwa ulinzi na usalama, kukua na kuimarika kwa biashara na shughuli zingine za kiuchumi na fursa ya kutumia rasilimali zilizopo kwa pamoja ikiwamo ardhi na bandari.

Alisisitiza kuwa serikali za pande mbili za Muungano zimeweka suala la kuuimarisha kuwa ni moja ya vipaumbele vyake na zinaendelea kushirikiana kwa pamoja kuhuisha na kuudumisha.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza fedha ambazo zilikuwa zitumike kwa ajili ya kuadhimisha Sikukuu ya Muungano zigawanywe pande zote mbili kwa ajili ya kusaidia miradi ya maendeleo.

"Kwa busara ya mama yetu (Rais Samia) baada ya kufanya uamuzi kwamba mwaka huu tuadhimishe Muungano wetu kwa kufanya kongamano, ameagiza fedha ambazo zilizokuwa zitumike kwa ajili ya sherehe mwaka huu zigawanywe kwenda pande zote mbili za Muungano na kila upande utaamua namna ya kuzitumia fedha hizo kwa ajili ya miradi ya maendeleo," alisema Dk. Mpango.

Akitoa mada katika kongamano hilo inayohusu historia ya Muungano na falsafa tofauti za aina mbalimbali za Muungano wa kisiasa duniani, Waziri wa Sheria na Katiba, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema: "Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni himilivu kwa sababu ni wa aina ya kipekee, ulikuwa ni Muungano wa hiari ndio maana umedumu. Muungano wa hiari katika nchi mbalimbali duniani imekufa, lakini huu (Tanganyika na Zanzibar) umebaki kwa sababu ni wa mshikamano na umoja."

Naye, Balozi Mohamed Hija Mohamed, akichangia mada hiyo alisema: "Muungano huu ulikuwa wa damu, tuliunganisha nafsi za undugu, kule Zanzibar kuna eneo linaitwa Mwera, ukifika pale utawakuta Wamakonde, Wasukuma. Ulikuwa ni muungano wa kifamilia zaidi kuliko wa kisiasa".

Naye Mhadhiri Msaidizi, Chuo cha Diplomasia, Abbas Mwalimu alisema: "Muungano huu una faida kiuchumi. Mzanzibar anawekeza Bara pasipo kufuata taratibu za uwekezaji kama wageni wengine. Pia wananchi kutoka Bara wengi wamewekeza Zanzibar, Muungano huu ni wa utegemezi wa kiuchumi."

# H/shauri zenye hati chafu mikononi mwa TAKUKURU

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Mohamed Mchengerwa ameagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupita kwenye kila Halmashauri zote ambazo zimepata hati chafu kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabuza Serikali (CAG) na kufanya uchunguzi.

Mchengerwa alitoa agizo hilo jana katika Wilaya ya Rufiji, alipokuwa kwenye ziara ya siku moja kuzungumza na watumishi wa halmashauri za Kibiti na Rufiji.

Alisema kuna haja kwa halmashauri hizo kufanyiwa uchunguzi ili kubaini watendaji wasio waaminifu na hatua za kisheria zichukuliwe.

Alisema halmashauri hizo zinatakiwa kufanyiwa uchunguzi ili ibainike sababu ya kupata hati chafu na waliohusika ili kuondoa watu ambao si waaminifu kwenye utumishi wa umma.

"TAKUKURU kwenye maeneo ambayo halmashauri zimepata hati chafu wafanye uchunguzi ili taarifa hizo zisaidie kuona sehemu ambazo hawakufanya vizuri na kama kuna uzembe, hatua zichukuliwe," alisema Mchengerwa. Mchengerwa pia aliwataka watendaji wa TAKUKURU kuhakikisha wanahudhuria kwenye mikutano inayoitishwa na wakuu wa wilaya kwenye maeneo yao ili watoe elimu kwa wananchi.

Aidha, Waziri huyo aliwataka viongozi wa taasisi za umma kushughulikia mashauri ya watumishi waliosimamishwa kazi waweze kupata haki zao kisheria.

Alisisitiza pia utolewaji wa mafunzo na semina kwa watumishi zitakazosaidia kuwajenga kuendelea kuwapa maadili wenye utumishi wao.

" Viongozi wa Taasisi, wakiwamo wakurugenzi tumieni ubunifu wenu kuwapatia mafunzo watumishi, zipo Taasisi ziko tayari kusaidia kutoa semina na mafunzo... wapeni fursa watumishi, hii inasaidia kushughulikia masuala ya maadili kazini tisizibe fursa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Patrick Sawala, alisema wilaya hiyo ina upungufu wa watumishi zaidi ya 800.

Alisema kuwa katika wilaya hiyo watumishi ambao wanaenda kinyume cha maadili walifukuzwa kazi ili kuimarisha utawala bora.

Alimwomba Waziri huyo kushughulikia kero zinazowakabili watumishi wa wilaya hiyo ukiwamo ukosefu wa usafiri na vitendea kazi katika kutekeleza majukumu yao.

# Waziri awasweka ndani mkurugenzi, mameneja Maji

**Na Neema Emanuel,** SENGEREMA

WAZIRI wa Maji, Juma Aweso, amewasweka ndani Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Maji Mwanza mkoani Mwanza, pamoja na mwakilishi wa mkandarasi anayejenga mradi wa maji wa Nyampande uliopo wilayani Sengerema, mkoani Mwanza.

Watendaji waliswekwa ndani ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Mwanza (MWAUWASA), Leonard Msenyele, Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Sengerema, Cassian Wittike, Meneja wa RUWASA Mkoa wa Mwanza, Immaculate Raphael, Meneja miradi wa MWAUWASA, Bogadi Mgwatu, Meneja wa Mamlaka ya Maji Sengerema, Robert Lupoja, pamoja na mwakilishi wa mkandarasi wa mradi huo.

Awali, akitembelea tanki la maji la Buswelu, linalojengwa kwa gharama ya Sh. Sh. bilioni 6, Waziri Awezo alimtaka mhandisi mshauri, Andrew Mwakagenda, kujitafakari baada ya kumdanganya kuwa wanafanya kazi hadi siku ya Jumapili.

Akizungumza baada ya kutembelea mradi huo, alisema hakuna kazi inayofanyika Jumapili bali aliwaleta wafanyakazi ili kuonyesha wanafanya kazi wakati hakuna wanachofanya.

"Hapa hakuna kazi mnayoifanya, kelele ni nyingi sana Mwanza, serikali inaleta fedha nyingi ili kukamilisha miradi ya wananchi kazi ifanyike kama hauwezi utupishe tunapokuja kukagua mradi msituuzie mbuzi kwenye gunia kwa kutuonyesha mnafanya kazi kumbe hamna mnachofanya tukiondoka na nyie mnaondoka,"alisema Aweso.

Aidha, aliiagiza MWAUWASA na RUWASA Mwanza washirikiane kuhakikisha wanakamilisha mradi wa Igongwe na Kahama kwa wakati ili wananchi wapate maji. Aliwataka washauri wote wa miradi ya maji kuacha maigizo bali wafanye kazi kwa bidii na kukamilisha kazi hiyo kwa wakati na watakaposhindwa kujipanga watasaidiwa.

Alisema azima ya Rais, Samia Suluhu Hassan ni kuona wananchi wanapata majisafi na salama hiyo ndio kiu yake, hivyo makandarasi wote watambue hakuna muda wa nyongeza, waache "janja janja" bali wachape kazi.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Leonard Msenyele alisema mradi wa Buswelu unatarajiwa kukamilika Oktober, mwaka huu.

Alisema kazi zilizopangwa kufanyika ni kulanza bomba la plastic na chuma kutoka kituo cha kusukuma maji Kiseke hadi tanki la Buswelu kilomita 9.51 kwa ajili ya wananchi zaidi ya 100,000.

Alisema uzalishaji wa maji jijini Mwanza kupitia mtambo wa Kapripoint unazalisha wastani wa lita million 90 kwa siku, huku mahitaji halisi yakiwa ni lita milioni 150 kwa siku, na kwamba kuna upungufu wa takriban lita milioni 60 kwa siku

Naye, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nadhifa Kemikimba, alisema Wizara itafuatilia utekelezaji kwa ukaribu kwani lengo lao ni miradi ikamilike kwa wakati.

## HABARI KITAIFA

# TUCTA yaiangukia serikali walioajiriwa Mei 2004

**Na Jumbe Ismailly** SINGIDA

SERIKALI imeombwa kuangalia upya uamuzi wake iliyofanya wakati wa kuwaondoa watumishi walioajiriwa Mei, 2004 kama itaona inafaa iwarejeshe kazini, na iwapo hawahitajiki kurejeshwa ni vyema ikawalipa haki zao zote wanazostahili.

Rais wa Shirikisho Huru la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Tumaini Peter Nyamuhokya, alitoa ombi hilo mjini Singida alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida na Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

Nyamuhokya ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), alisisitiza kwamba kama serikali ina uwezo wa kurudi kusikiliza upya watumishi walioajiriwa baada ya Mei 2004 ni wafanyakazi halali kwani waliajiriwa kihalali na kuingizwa kwenye mfumo na kuendelea kulipwa mishahara.

"Hawajadanganya chochote na serikali imewatoa kazini, haikuwalipa chochote wala kuwarudisha makwao wala wapi, hivyo walitazame upya na walibebe hili jambo hata kwenye risala yetu lipo na tutaendelea kulisemea,"alisisitiza Nyamuhokya.

Kwa mujibu wa Rais huyo wa Tucta, watumishi hao walioondolewa walionewa, hivyo wanatakiwa kurejeshwa na kama watakuwa wanawaacha, basi wasisite kuwalipa haki zao zote, huku akikiri kushindwa kuwasemea watumishi walioghushi vyeti vya elimu.

"Wale ndugu zangu na mimi ambao kidogo tulikarabati vyeti au tulichonga vyeti vya bandia tunashindwa kusemea uovu, maana kuna uovu umetendeka nyuma ya hili jambo, na hili jambo tulishalisogeza mpaka kwenye taasisi zetu za kimataifa kule ILO (Shirika la Kazi Duniani), walituambia haiwezekani na hatuwezi kusaidia jambo hilo." alisema.

# Usajili VICOBA mwisho Ijumaa

**Na Salome Kitomari**

MWISHO wa usajili wa vikundi vidogo vya huduma ndogo za fedha (VICOBA) ni Ijumaa (Aprili 30, mwaka huu), kwa kusajiliwa mtandaoni.

Awali, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ilitoa muda hadi Novemba 31, mwaka 2020, lakini aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alitangaza kusogeza mbele hadi Aprili 30, mwaka huu.

Usajili huo ulisimama kwa muda ili kutoa nafasi kwa Maofisa Maendeleo ya Jamii na wataalam wa TEHAMA kupewa elimu ya kutumia mfumo wa usajili kielektroniki.

"Tunashauri vikundi vyote vichangamkie fursa hii ya usajili kwa mujibu wa sheria kwa kuwa serikali ina malengo mazuri kurasimilisha, ili viendelee kutoa mchango mkubwa kwa wanachama wake na kumkomboa mwananchi wa kawaida kutoka kwenye umaskini hadi hali nzuri zaidi," alibainisha.

Meneja wa Huduma Ndogo za Fedha na Maduka ya Kubadilisha Fedha, Victor Tarimu, alisema faida za usajili wa vikundi vidogo vya huduma ndogo za fedha kuwa ni pamoja na kunufaika na mikopo ya uwezeshwaji inayotolewa na serikali.

Alisema serikali ina mifuko mingi ya kusaidia wananchi na hivyo ni rahisi kupata misaada kutoka kwenye taasisi za serikali kwa kuwa vikundi na kwamba ni muhimu kuwatoa watu katika umaskini na kwenda kwenye hali nzuri zaidi.

Alisema vikundi vikisajiliwa vitakuwa na nguvu ya kisheria na kurahisisha kupata mikopo kwenye benki na ufadhili kwa sababu vinakuwa vinavyotambulika rasmi.

"Sheria imeweka bayana kuwa ni lazima vikundi vyote vipate elimu ya fedha kwa sababu vingi havifanyi vizuri kwa kukosa elimu ya fedha, watoa huduma katika vikundi na wanaotumia huduma hawana elimu wanafanya miamala ya kifedha bila uelewa na kushindwa kupata faida inayotakiwa," alisema Tarimu.

Pia, BoT ilisisitiza kuwa usajili ni bure kwa kuwa gharama za usajili zimebebwa na serikali na wanachopaswa ni kwenda serikali za mitaa kwa ajili ya kupata utambulisho na baadaye halmashauri ambako kuna Ofisa Maendeleo ya Jamii.

**MATAKWA YA KANUNI**

Kwa mujibu wa kanuni ya 4 hadi 7 ya mwaka 2019, watoa huduma ndogo za fedha, wanachama wa VICOBA wanatakiwa kufanya mkutano wa awali, kuwa na kamati ya mpito na majukumu yake na kikao cha uanzishaji na majukumu yake.

Kanuni ya 8 hadi 17 ni maombi ya usajili yakiambatana na nakala ya katiba yenye sahihi za wanachama, nakala za muhtasari ya mkutano wa uanzishaji, maazimio ya wanachama kuanzisha kikundi.

Vinatakiwa kuwa na mapendekezo ya muundo wa kikundi, uthibitisho wa malipo ya michango ya awali, barua ya mamlaka ya kata au kijiji, na jina la kikundi lijumuishe maneno 'kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii' na baada ya kukamilisha wanakikundi watatakiwa kufanya kikao cha kwanza ndani ya mwezi mmoja.

**"Tunashauri vikundi vyote vichangamkie fursa hii ya usajili kwa mujibu wa sheria kwa kuwa serikali ina malengo mazuri kurasimilisha, ili viendelee kutoa mchango mkubwa kwa wanachama wake na kumkomboa mwananchi wa kawaida kutoka kwenye umaskini hadi hali nzuri zaidi," alibainisha.**


SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC)



Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere
Rais wa kwanza wa Tanzania



Mhe. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



Dr. Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Zanzibar



Hayati Sheikh Abeid Amani Karume
Rais wa Kwanza wa Zanzibar

MIAKA 57 YA MUUNGANO

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania tunaungana na Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar pamoja na Watanzania wote kusheherekea sikukuu ya Miaka 57 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

*TASAC tunaendelea kudhibiti usafiri wa njia ya maji na kufanya biashara ya huduma za meli.*

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania: Anwani/Mahali P.O. Box 989, Dar es Salaam,Tanzania Simu ya Msaada: +255 22 2127314, Nukushi: Nō: +255 22 2127313, Barua pepe: info@tasac.go.tz



Baadhi ya wajumbe wakifatilia mada kwenye mkutano wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania(CTI) jijini Dar es Salaam mwisho mwa wiki, kujadili changamoto zinazoikabili sekta ya viwanda na kuja na mapendekezo yatakayosaidia kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtandao wa wanawake wampongeza Rais Samia

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MTANDAO wa wanawake, katiba, uongozi na uchaguzi, kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya usawa wa jinsia na haki za wanawake nchini wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuonyesha fursa za kukuza uchumi.

Aidha, matokeo chanya ya maendeleo yatakayosababisha kukua kwa misingi inayojumuisha usawa wa jinsia.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP - Mtandao), Lilian Liundi, alisema Rais anastahili pongezi kwa ahadi ya kulinda misingi ya demokrasia na uhuru wa watu. Alisema rais ameona fursa kubwa ya kujenga misingi na mikakati ambayo haitaacha nyuma ushiriki na sauti za wanawake kama wanajamii wa taifa utaleta ufanisi mkubwa. Alimuomba Rais Samia kukutana na vyama vya siasa, kuwe na msisitizo wa kuhakikisha mkakati wa usawa wa jinsia na demokrasia ndani ya vyama inatekelezwa kama ajenda yao kimkakati.

Kwa mujibu wa Liundi, kipaumbele cha kuboresha sekta ya madini, utalii na nyingine ni cha kupongezwa na kwamba kwa bahati mbaya kwa muda mrefu sekta hizo zimekuwa zikitoa kipaumbele na kuwanufaisha zaidi wanaume kuliko wanawake. Alisema TGNP inaamini kuwa utekelezaji wa ahadi hizo kuhakikisha wanawake wananufaika, ikiwamo kufungamanisha maendeleo ya kilimo na viwanda kwa lengo la kuwezesha mazao ya kilimo yatumike kama malighafi za viwanda.

Liundi alisema suala la kutoa kipaumbele katika uwekezaji, na umiliki wa ardhi ni nyeti na tete ambalo linahitaji umakini mkubwa na alimpongeza rais kwa kuainisha kipaumbele hicho na kuahidi kuwa ushiriki wa wanawake katika suala hilo ni wa muhimu kwa sababu ardhi imekuwa msingi mkuu wa ushiriki wa wanawake katika maendeleo.

Vile vile alisema kuongeza usawa wa kijinsia kwa kuongeza wanawake katika nafasi za uongozi kwa kuzingatia vigezo na sifa stahiki kutasaidia kupunguza pengo la usawa wa kijinsia katika nafasi za uongozi na kuongeza tija katika kuingiza masuala ya kijinsia katika sera, bajeti, mipango na michakato yote ya maendeleo na kuongeza kasi ya maendeleo jumuishi na endelevu nchini.

Eneo jingine, kupunguza vifo vya wajawazito na watoto na kuimarisha huduma za afya kwa kujenga miundombinu, kuongeza watumishi, vifaa tiba, dawa na vitendanishi, pamoja na kuboresha bima ya afya kwa wazee na kwa wote kutawasaidia wanawake kwa kuwa ndio wanaobeba mzigo mzito katika masuala ya afya katika familia na jamii kwa ujumla. Kwa mujibu wa Liundi, kuongeza uwajibikaji wa watendaji katika miradi ya maji, kuhakikisha upatikanaji wa maji sehemu zisizo na maji kwa kupitia mabwawa ya kuvuna maji ya mvua na kuimarisha kamati za maji za mitaa na vijiji.

Eneo jingine ambalo TGNP waliona ni muhimu ni kukuza uchumi na kupambana na umaskini nchini, kupambana na rushwa na ubadhilifu wa mali ya umma, ulipaji wa kodi usio na bughudha, kukuza na kuongeza tija katika sekta ya kilimo na mifugo.

Pia kukuza ajira na mapato kwa kukuza na kulinda sekta ya Madini, utalii, viwanda na kwingineko, kuendeleza na kukuza miundombinu mbalimbali, kuboresha na kuleta mapinduzi zaidi ya teknolojia, TEHAMA na mawasiliano, kuongezea uwekezaji katika sekta za nishati, elimu na afya.

# Tril. 11.4/- zaokolewa kesi dhidi ya serikali

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

OFISI ya Wakili Mkuu wa Serikali imeokoa Sh. trillioni 11.4 kutokana na kesi za ndani na nje ya nchi za madai mbalimbali ya fidia kutokana na miradi mbalimbali.

Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, alibainisha hayo wakati akifungua mafunzo ya siku nne yalianza jana mjini Morogoro kwa mawakili na watumishi wa ofisi hiyo. Mafunzo hayo yaliyotolewa na majaji wastaafu wa Mahakama Kuu yamelenga kuwajengea uwezo wa namna ya kuendesha usuluhishi wa mashauri yanayofunguliwa kwa serikali ndani na nje ya nchi. Malata alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kulikuwa na kesi zinazohusisha masuala ya fedha ambazo serikali ilipaswa kulipa kama fidia, lakini kwa kutumia ofisi hiyo iliweza kupambana vilivyo na kuhakikisha serikali inashinda kesi hizo. Alisema kuwa serikali ilifunguliwa jumla ya kesi 3715 za ndani ya nchi ambazo 451 zilisikilizwa zikihusisha na kesi nyingine ambazo sio za madai ya fedha na kushinda asilimia 95.

Alisema kati ya kesi hizo zilizosikilizwa ambazo wameshinda zina jumla ya thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 700 na kesi ambazo hawakushinda zina thamani ya Sh. bilioni 20 na kwamba hata hivyo, ofisi hiyo imezikatia rufani. Kwa upande wa kesi iliyofunguliwa hivi karibuni dhidi ya serikali nchini Marekani ya fidia ya Dola za kimarekani milioni 55 sawa na Sh. bilioni 100 za Tanzania, alisema kupitia ofisi hiyo wameshinda kesi hiyo.

Alisema kesi hiyo ilifunguliwa na familia ya Vallambia ambayo inaishi nchini Marekani,ilikuwa ikidai fidia ya kiasi hicho cha fedha baada ya kuingia mkataba wa ununuzi wa vifaa na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alifafanua kuwa katika mkataba huo serikali ilitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba, lakini upande wa hiyo familia ikaona kuna upungufu katika utelezaji wa mkataba, hivyo kuamua kufungua kesi hiyo Marekani.

Alisema kuwa kesi hiyo ambayo serikali imeshinda ni miongoni mwa kesi nne zilizofunguliwa nje ya nchi ambazo ofisi hiyo inaendelea kuzitetea na kufanya mashauriano na wahusika.

Hata hivyo pamoja na mafanikio hayo, aliwaonya watumishi wa ofisi hiyo kutobweteka na mafanikio hayo bali waongeze juhudi katika kazi hiyo na kwamba watakaofanya uzembe au kutowajibika na kusababisha hasara kwa serikali, hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali,Dk. Boniphace Luhende, alisema mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo mawakili wa serikali katika mashauri ya usuluhishi katika masuala ya kitaifa na kimataifa.


**UPOTEVU WA CHETI:**



**Justinian Ikingura,** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba BMS 115/40,** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary KAHORORO Mwaka 1974,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa
**DAR/CHU/RB/208488/2021**

## TANGAZO LA MNADA

**TAN-GLOBAL VENTURES COMPANY LIMITED** kwa idhini iliyopewa na **NATIONAL BANK OF COMMERCE (NBC)** itauza kwa mnada wa hadhara nyumba zilizo orodheshwa kwenye jedwali katika maeneo husika:

| ACCOUNT NAME | PLOT NO. | PLOT LOCATION | BRANCH |
|---|---|---|---|
| New Nandope Guest House | CT NO.39356, LO NO.128801, PLOT NO.120, BLOCK 'A', POLICE MTWARA TOWNSHIP I.N.O ALLY ABDUL LEMU. | POLICE-MTWARA | Mtwara |
| Jeremiah F. Manyiwa | C.T NO. 40920-LR MWANZA, L.O. NO. 479552, PLOT NO. 439, BLOCK 'L' KANYENYE AREA, TABORA MUNICIPALITY I.N.O. IDDY RAMADHANI SHABAN | KANYENYE AREA, TABORA | TABORA |
| Twahiru H Semtindi | C.T.NO.23363-LR MOSHI, L.O. NO. 171445, PLOT .NO. 1116, LUKOZI AREA, LUSHOTO DISTRICT I.N.O SHAURI ATHUMANI SEMTINDI. | LUKOZI TANGA | TANGA |
| Lasway Truck | Plot No.35-36, Block “KKK”, Karanga, Moshi | KARANGA MOSHI | MOSHI |
| MALOBENI TRADERS COMPANY LTD | CT NO.55664, L.O. NO.205318, PLOT NO.82/1 BLOCK 'A' UBUNGO KIBANGU AREA I.N.O SIMON ABEL MBATIANI. | UBUNGO - DAR ES SALAAM | UBUNGO |
| Razu Fashion Investm | TITLE DEED PROPERTY SITUETED OVER PLOT NO 2076 BLOCK D AT CHANGANYIKENI AREA WITH CT NO 84171 IN THE NAME OF VENANCE PETER KIMBORI | CHANGANYIKENI -DAR | Victoria |
| PELICAN SAFARIS | CT NO.16274-LR MOSHI, L.O. NO.178537, FARM NO.1220 OLTULELEI VILLAGE, ARUMERU DISTRICT I.N.O OLAIS THEOLIO METILI. | ARUMERU DISTRICT | ARUSHA |
| OSMUND WILLIAM MAPUNDA | C.T NO. 5435 MTW, L.O. NO. 300099, PLOT NO. 399 BLOCK '2' LIGULA AREA,MTWARA MUNICIPALITY I.N.O OSMUND WILLIAM MAPUNDA. | LIGULA-MTWARA | Mtwara |
| MAKINYO ENTERPRISES | CT NO.9680-MBYLR, L.O NO.173140, PLOT NO.94 BLOCK "R" HIGH DENSITY, KATANDALA AREA,SUMBAWANGA TOWNSHIP I.N.O JOSEPH | KATATANDALA-SUMBAWANGA | Sumbawa nga |
| SUPERB BUSINESS SERVICES LIMITED | CT NO.137576, L.O. NO 483908, PLOT NO.2140, BLOCK 'E' GONGO LA MBOTO AREA, ILALA MUNICIPALITY I.N.O HERIAMINI JONATHAN MGHASE. | GONGOLAMBOT O-DAR | Corporate |
| YUSSUF KHAMIS MOHAMMED | REG NO.140 OF 2003, VOL 1 OF BOOK A-3, DATED 5TH MARCH 2013, KINUNI AREA-WESTERN DISTRICT, ZANZIBAR I.N.O YUSSUF KHAMIS MOHAMMED. | ZANZIBAR | Zanzibar |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Nyumba tajwa hapo juu zitauzwa kwa mnada wa hadhara baada ya wiki mbili ya tangazo hili endapo walengwa hawatalipa madeni yao ndani ya muda huo.
2. Mnunuzi aliyeshinda anatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano(25%) mara tu baada ya mnada kufungwa,na atakamilisha asilimia sabini na tano(75%) baada ya siku kumi na nne(14),Fedha hiyo isipolipwa ndani ya muda huo mnada utarudiwa bila kurudishiwa fedha ya awali.

**Mkurugenzi Mtendaji**

**Imetolewa leo tarehe 27/04/2021 na TAN-GLOBAL VENTURES CO.Ltd, S.L.P 612, TANGA, abrahamshempemba@gmail.com 0715-752205, 0714-560080, 0692-693410**

# Tanzania yavuka lengo la chanjo

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA imefanikiwa kwa asilimia 98 ya kiwango cha utoaji chanjo aina tofauti kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo na kuvuka lengo lililowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) la asilimia 90.

Mkurugenzi wa Kinga kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, akizungumza kuhusu maadhimisho ya wiki ya chanjo inayoanza Aprili 24 hadi 30, kila mwaka.

Alisema mafanikio ya utoaji chanjo hususan kwa walio chini ya miaka miwili, imesaidia kutokomeza magonjwa na kupunguza athari za maradhi ikiwamo Polio.

"Tunawalenga watoto ambao hawajakamilisha kupata ratiba ya chanjo au kuipata, wafike vituo vya huduma za afya katika wiki hii, sababu ni wiki ya hamasa, ingawa huduma ya chanjo itaendelea kama kawaida hata baada ya wiki ya chanjo," alisema.

Dk. Subi alifafanua kuwa miaka 15 iliyopita kulikuwapo kambi za wodi za wagonjwa wa surua na kwamba hivi sasa hazipo tena, kutokana na mafanikio ya chanjo.

Alibainisha kuwa Novemba, mwaka 2015 Tanzania ilipata cheti cha mafanikio ya utoaji chanjo, pia pepopunda tangu mwaka 2012 ilifanikiwa kutokomeza ugonjwa huu kwa watoto, vilevile ipo katika hatua za kuondoa rubella na surua.

"Vifo vya watoto vimepungua, tuna chanjo za aina tisa kwa ajili ya kinga dhidi ya magonjwa 13, zisipochanjwa ipasavyo itahatarisha maisha ya watoto," alisema Dk. Subi.

Pia, alisema maadhimisho hayo yatafanyika mikoa yote kwenye vituo vyote kwa kutoa chanjo kwa watoto na elimu kwa wazazi pamoja na walezi.

# NMB yatenga bil. 5/- mikopo ya bodaboda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ( Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amewataka madereva wa pikipiki za abiria maarufu bodaboda kujiwekea heshima ili watambulike katika ajira rasmi na kukopesheka.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizindua mfumo wa kukopesha pikipiki kutoka Benki ya NMB, NMB MASTABODA MILIKI CHOMBO jijini Dodoma.

Alibainisha kuwa uongozi wa Benki ya NMB umefanya kitu kikubwa kwa kuwakumbuka madereva wa bodaboda na kubainisha kuwa wanawagusa wateja wadogo wenye mahitaji makubwa katika huduma zao.

"Rais Samia Suluhu Hassan, anasema kila mmoja ashiriki katika kukuza uchumi wa nchi kwa kufanya kazi, hivyo hata nyinyi waendesha bodaboda mnao wajibu wa kufanya kazi na kulinda nidhamu. Nadhani mnafahamiana, wale wakorofi wanaowaharibia sifa zenu pia mnawafahamu," alisema Mhagama na kusisitiza:

"Lindeni heshima yenu ili jamii iwaheshimu. Isiwachukulie kama watu msio na ajira rasmi. Ndio maana ninaziomba taasisi nyingine za kifedha ziige mfano wa Benki ya NMB kuwakumbuka watu wa chini, wawakumbuke waendesha bodaboda nchi nzima muweze kukopesheka nanyi mmiliki pikipiki zenu badala ya kuendelea kuwatumikia watu wengine."

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema utekelezaji wa NMB Mastaboda- Miliki Chombo ni matokeo ya agizo alilolitoa Waziri Mhagama Oktoba, 2019 alipokuwa mgeni rasmi kwenye kampeni ya kulipia nauli ya bodaboda kwa kutumia mfumo wa MasterCard QR iliyoitwa MastaBoda.

"Itakumbukwa Mheshimiwa Waziri wakati ukizindua utaratibu wa kulipia nauli za bodaboda kwa kutumia mfumo wa QR Card, ulituagiza tuweke utaratibu wa kuwakopesha pikipiki hawa madereva wa Bodaboda. Tulikaa tukajadiliana tukaamua kuja na wazo hili, tunafahamu kuna zaidi ya waendesha Bodaboda milioni mbili nchini, lakini hawapo kwenye mfumo rasmi wa kibenki na wengine hawana ajira rasmi. Tunaamini utaratibu huu utawaleta pamoja na watatambulika kama watu wenye ajira rasmi," alisema Zaipuna.

Alibainisha kuwa, dereva wa bodaboda atakayekuwa kwenye kikundi na kufuata taratibu za kutambulika kisha akakopeshwa pikipiki na Benki ya NMB, maana yake atakuwa miongoni mwa wateja wao na pia atamiliki chombo chake, hiyo tayari atakuwa katika ajira rasmi ambapo wapo watakaomiliki pikipiki zaidi ya moja za miguu miwili na mitatu.

"Kwa kuanzia tunaanza na madereva wa bodaboda wa Dar es Salaam, tumewatengea Sh. Bilioni 5 kwa kumalizia mwaka huu. Mwitiko ukiwa mkubwa tutaongeza fedha kwa kadiri ya mahitaji. Tunataka kuja na mbinu nyingi za ubunifu zaidi ili kukuza uchumi na kuongeza ajira hasa kwa vijana," alisema Zaipuna.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Biashara Ndogo na za Kati Benki ya NMB, Filbert Mponzi, alisema utaratibu ulivyo kwanza dereva wa bodaboda atatakiwa kufungua akaunti ya NMB kama hana, kisha atasubiri ndani ya miezi mitatu huku akiendelea kufanya miamala ili kuwa na sifa za kukopesheka.

"Kikubwa tunataka mteja awe na kitambulisho cha taifa kuonyesha ni raia lakini pia kuwa na leseni ya udereva, tayari tumeshakutana na madereva wa bodaboda 5,000 kwa Mkoa wa Dar es Salaam tumewapa mafunzo. Kwa kuwa ili upate mkopo lazima upewe elimu namna ya kuutumia na nidhamu ya kutunza fedha," alisema Mponzi.

Naye, Mwenyekiti wa Madereva wa Bodaboda Mkoa wa Dar es Salaam, Jackob Massawe, aliishukuru benki hiyo ni kwa kuwakumbuka kila wakati na kuahidi watautendea haki mkopo huo ili wasiwaangushe.



# FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

1st Housing

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.03.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31st Mar. 2021 | Robo Mwaka iliyopita 31st Dec. 2020 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 92 | 2 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,657,426 | 2,542,147 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 6,386,865 | 8,921,407 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 7,961,296 | 6,254,136 |
| 12 | Mali Nyingine | 549,167 | 585,857 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 587,637 | 247,025 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **20,764,484** | **20,172,574** |
| | | | |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 418,073 | 413,087 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 801,510 | 665,547 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 121,749 | 87,558 |
| 27 | Dhima Nyingine | 417,580 | 11,712 |
| 28 | Madeni | 1,010,274 | 1,010,479 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **2,769,186** | **2,188,383** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **17,995,297** | **17,984,191** |
| | | | |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,911,640) | (3,424,069) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 11,106 | (487,571) |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 38 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **17,995,297** | **17,984,191** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 133,564 | 137,137 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 19,465 | 38,608 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 86.66% | 88.78% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.68% | 2.18% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 1957.04% | 1550.44% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 38.34% | 31.18% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 90.35% | 80.99% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1.21% | 0.00% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.93% | 4.89% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Maelezo | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31st Mar. 2021 | 31st Mar. 2020 | 31st Mar. 2021 | 31st Mar. 2020 |
| 1 | Mapato ya Riba | 521,782 | 361,596 | 521,782 | 361,596 |
| 2 | Gharama za Riba | (28,556) | (7,625) | (28,556) | (7,625) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **493,227** | **353,971** | **493,227** | **353,971** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 9,571 | (258) | 9,571 | (258) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **36,227** | **1,370** | **36,227** | **1,370** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 26 | (1,080) | 26 | (1,080) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 36,198 | 2,450 | 36,198 | 2,450 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 2 | - | 2 | - |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(525,128)** | **(527,837)** | **(525,128)** | **(527,837)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (233,488) | (237,165) | (233,488) | (237,165) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (291,640) | (290,671) | (291,640) | (290,671) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **13,896** | **(172,754)** | **13,896** | **(172,754)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (2,790) | - | (2,790) | - |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **11,106** | **(172,754)** | **11,106** | **(172,754)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **11,106** | **(172,754)** | **11,106** | **(172,754)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 18 | 10 | 18 | 10 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.05 | (0.79) | 0.05 | (0.79) |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.05% | -0.88% | 0.05% | -0.88% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.06% | -0.94% | 0.06% | -0.94% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 99.18% | 148.54% | 99.18% | 148.54% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.73% | 2.05% | 2.73% | 2.05% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo ya mwaka ya sasa (31.03.2021)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya mwaka (01.01.2021)** | **21,800,000** | **-** | **(3,911,640)** | **-** | **-** | **95,831** | **17,984,191** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 11,106 | - | - | - | 11,106 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.03.2021)** | **21,800,000** | **-** | **(3,900,534)** | **-** | **-** | **95,831** | **17,995,297** |
| | | | | | | | |
| **Robo ya mwaka iliyopita (31.12.2020)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka (01.10.2020)** | **21,800,000** | **-** | **(3,826,875)** | **-** | **-** | **95,831** | **18,068,956** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (84,765) | - | - | - | **(84,765)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.12.2020)** | **21,800,000** | **-** | **(3,911,640)** | **-** | **-** | **95,831** | **17,984,191** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2021

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31st Mar. 2021 | 31st Dec. 2020 | 31st Mar. 2021 | 31st Mar. 2020 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **13,896** | **(84,765)** | **13,896** | **(172,754)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 77,389 | 128,936 | 77,389 | 129,289 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,707,160) | (1,323,684) | (1,707,160) | (971,398) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 4,986 | - | 4,986 | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (1,115,279) | (2,542,147) | (1,115,279) | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 573,233 | (1,544) | 573,233 | 10,901 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 36,690 | 52,084 | 36,690 | (74,637) |
| | - Kodi iliyolipwa | - | - | - | - |
| | - Mengineyo | 30,347 | 97,541 | 30,347 | (6,700) |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(2,085,899)*** | ***(3,673,580)*** | ***(2,085,899)*** | ***(1,085,299)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (418,001) | - | (418,001) | (1,600) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(418,001)*** | ***-*** | ***(418,001)*** | ***(1,600)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (205) | 1,010,479 | (205) | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (49,489) | (73,409) | (49,489) | (75,251) |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***(49,695)*** | ***937,070*** | ***(49,695)*** | ***(75,251)*** |
| | | | | | |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na** | **(2,553,594)** | **(2,736,510)** | **(2,553,594)** | **(1,162,150)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 8,921,408 | 11,657,918 | 8,921,408 | 14,965,937 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | 19,143 | - | 19,143 | (71,889) |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **6,386,957** | **8,921,408** | **6,386,957** | **13,731,898** |

### MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES

| S/No | ITEMS | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| 1 | Prime Lending Rate (PLR) | 16% p.a. |
| 2 | Maximum spread above PLR | 4% p.a. |
| 3 | Application Fee (Non-refundable) | TZS 200,000/- |
| 4 | Processing Fee | 1.5 % of the loan value |
| 5 | Facility Fee | 1.5 % of the loan value |
| 6 | Valuation Fee | Paid by the client as per the invoice |
| 7 | Legal Fee | Paid by the client to FHF account and FHF will pay law firm |
| 8 | Early Repayment | 5% of the amount to be prepaid |
| 9 | Annual Review Fee | NIL |
| 10 | Cheque returned Unpaid (Outward & Inward) | TZS 50,000/- |
| 11 | Loan Statement | TZS 20,000/- |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| Jina na Cheo : | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Sasa M. Chonza **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | (Imesainiwa) | 25.04.2021 |
| Amulike Kamwela **(Mkuu wa Fedha)** | (Imesainiwa) | 25.04.2021 |
| Derrick Rushekya **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | (Imesainiwa) | 25.04.2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| Jina: | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Sanjay Suchak **Mwenyekiti** | (Imesainiwa) | 25.04.2021 |
| Charles Itembe | (Imesainiwa) | 25.04.2021 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utekelezaji ahadi mazingira bora uwekezaji uharakishwe

**KILIO** cha mazingira yasiyo rafiki kwa wawekezaji kimekuwa kikitolewa kila uchao, huku mamlaka mbalimbali za serikali zikiahidi kukitafutia ufumbuzi.

Kimsingi, wawekezaji wa nje na ndani wamekuwa wakilalamikia vikwazo kadhaa vinavyowakatisha tamaa, hivyo kufikia mahali kusitisha uwekezaji wao.

Vikwazo kadhaa ambavyo vilikuwa vikilalamikiwa na wawekezaji ni urasimu, rushwa, kuchelewa kutoa vibali na leseni, vibali vya ardhi, viwango vya kodi visivyotabirika na mambo mengine mengi yanayofanana na hayo, hivyo kukinzana na nia ya dhati ya serikali katika kuvutia uwekezaji, ambao ni moja ya mikakati ya kuliwezesha taifa letu kusonga mbele kiuchumi.

Bila taifa kuvutia na kuwa na wawekezaji haliwezi kusonga mbele, kwa kuwa wawekezaji wana mitaji, wana teknolojia, wana uzoefu katika suala zima la masoko na pia ni watengenezaji wa ajira nyingi katika sekta binafsi.

Kwa hiyo kutowajali na kuwawekea mazingira bora wawekezaji, taifa husika litakuwa linajidanganya, kwa kuwa mwishowe umasikini utaendelea kuwaandama na kuwatesa wananchi.

Hata hivyo, wiki iliyopita serikali ya awamu ya sita ilitangaza kwamba italipatia kipaumbele suala hilo, ambapo Rais, Samia Suluhu Hassan alipokuwa akilihutubia Bunge Alhamisi, alisema kuwa serikali yake itahakikisha inaendelea kufanya maboresho kwenye sera na sheria kwa lengo la kuondoa vikwazo kwa wawekezaji.

Rais Samia kadhalika, alisema serikali itawapa vivutio wawekezaji, kushughulikia vibali vya kazi pamoja na kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) kuanzisha mfumo wa kushughulikia kwa pamoja kero za wawekezaji.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, ameahidi kufanya mabadiliko kwenye Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) sambamba na kuongeza ufanisi katika kuimarisha mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kikao chake na menejimenti na wafanyakazi wa TNBC wiki iliyopita, Mwambe alisema baraza kama taasisi ni kiungo muhimu kati ya sekta za umma na binafsi na hivyo kuimarika kwake kutaleta matokeo chanya ikiwamo kukua kwa biashara na kuongezeka kwa uwekezaji.

Alisema licha ya uchanga wa wizara, yeye na timu yake watahakikisha wanashirikiana na wadau wote katika sekta za uwekezaji, biashara na taasisi zote zilizopo kwenye wizara hiyo kuweka mikakati ya namna bora ya kuvutia zaidi uwekezaji na biashara.

Kero za wawekezaji nchini sio jambo jipya, hivyo kinachotakiwa sasa ni serikali kuitekeleza ahadi yake hiyo kwa vitendo ili nchi yetu ipate wawekezaji wengi na makini wenye nia ya dhati ya kuwekeza hivyo kuchochea uchumi na kuboresha maisha ya Watanzania.

Katika kutimiza lengo la kuwavutia na kuwaondolea kero wawekezaji, tunaishauri serikali iangalie upya utendaji wa mamlaka zinazogusa uwekezaji kama Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Kadhalika, tunaishauri serikali kuwa makini wakati wa kutoa vibali kwa wawekezaji; kwa kuhakikisha wanaopewa ni wenye vigezo vinavyokidhi sifa za uwekezaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Rais ameelekeza sasa kazi zianze

Na Sabato Kasika

**ELIMU** ya kujitegemea, kwa kawaida hailengi nadharia au ujuzi tu, bali pia namna ambavyo mtu anaweza kufaidika nayo kiuchumi na kumudu maisha yake.

Hiyo ni kwa sababu, elimu ni mkusanyiko wa stadi, maarifa na ujuzi anaokuwa nao mtu baada ya kuupata kwa njia mbalimbali, rasmi na zisizo rasmi ili kumwezesesha kumudu mazingira yanayomzunguka na kubadilisha changamoto kuwa fursa.

Mara baada ya Tanzania kupata uhuru mwaka 1961, Mwalimu Julius Nyerere, alifanya jitihada mbalimbali ikiwamo kuboresha elimu ili iwe ya kujitegemea.

Katika hilo, falsafa yake ilikuwa ni elimu ya kujitegemea ili kwamba, kila mwanafunzi anapohitimu shule au chuo awe na ujuzi wa kumwezesha kudumu maisha kutokana na ujuzi alioupata masomoni.

Hata hivyo, mambo yanakwenda yakibadilika na sasa badala ya wahitimu kutumia ujuzi waliopata vyuoni, sasa wamekuwa wakizunguka katika ofisi na katika kampuni mbalimbali kutafuta ajira.

Kutokana na wingi huo wa wahitimu kutegemea kuajiriwa, mtindo huo unaelezwa na wataalamu na wanaharakati kuwa kuna haja ya kubadili mfumo wa elimu uliopo sasa, kwa kuwa unashindwa kumuandaa mwanafunzi kujitegemea.

Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi inashauriwa kuangalia upya mfumo huo wa elimu, kwa lengo la kupata ule ambao utakuwa na manufaa kwa wanafunzi hasa elimu-ujuzi.

Hayo ni miongoni mwa mambo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan, anayataja katika hotuba zake mbalimbali kwa vile mfumo wa elimu ikibadilishwa kama ambavyo anataka na kujikita zaidi katika elimu ya ujuzi, watapatikana wahitimu watakaoweza kutumika katika sekta mbalimbali za kiuchumi ambao si lazima waajiriwe.

Kama ambavyo anaelekeza anataka mfumo huo kuangaliwa upya huku akivitaka pia vyuo kutoa elimu yenye ujuzi na ushindani itakayowawezesha wanafunzi kupata ajira kwa haraka, hilo ni jambo la msingi.

Hatua hiyo inaweza kuondoa tatizo la wanafunzi kuhitimu vyuo na kuzunguka na vyeti katika ofisi mbalimbali kutafuta ajira, badala yake watajiajiri au kama watakuwa na ujuzi, itakuwa ni rahisi kuajiriwa pale nafasi itakapopatikana.

Kimsingi, dunia imebadilika, waajiri wanategemea kupata wafanyakazi wenye ujuzi na kuwashindanisha, hivyo ni wazi kwamba, suala la kuwapo kwa elimu-ujuzi nchini lina umuhimu wake.

Hivyo vijana kama nguvukazi ya taifa, wakiwamo wasomi wanaohitimu vyuo mbalimbali, si vibaya kuwandaa, kwa kuwa katika taifa lolote wana mchango kwenye ukuzaji wa uchumi na maendeleo ya jamii.

Hapa nchini, kuna mfumo wa elimu ya awali hadi chuo kikuu ikiwa imegawanyika katika miaka mbalimbali ambayo mwanafunzi anatakiwa kusoma ili kupata stadi zinazohusika. Mfumo huo umewekwa kwa mujibu wa mtaala wa elimu, ambao sasa inashauriwa ufanyiwe marekebisho ili usaidie wanafunzi kuwa na ujuzi wa kuwawezesha kujiajiri wanapohitimu vyuo.

Inasikitsisha kuona vijana wengi wakihitimu elimu katika vyuo vikuu na vile vya kati wakilundikana mitaani na malalamiko ya ukosefu wa ajira pamoja na stadi za maisha ikiwamo kujiajiri na ujasiriamali.

Kwa sasa serikali inagharamia elimu na inachangia kuwapo kwa wahitimu wengi, hivyo suala la uboreshaji wa elimu ambayo itawapa ujuzi wahitimu kujiajiri au kujitegemea lina umuhimu wake.

Kikubwa anachokitaka Rais ni kuwawezesha wahitimu kuwa na ujuzi ili waweze kujitegemea, na hivyo kupunguza wimbi la wasomi kuzurura mitaani bila kazi, lakini pia waweze kuingia kwenye soko la ajira.

Ubora wa elimu shuleni au vyuoni ukiambatana na ujuzi, hivyo kama ambavyo anatamani iwe, ni vyema wizara husika ikaangalia namna ya kuwanoa wanafunzi ili wanapohitimu wawe na ujuzi.

## TANGAZO

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 31-Mach-2021 | Robo Mwaka iliyopita 31-Dis-2020 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 786 | 616 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 2 926 | 4 727 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 39 | 90 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 181 | - |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | 202 | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 5 000 | 8 300 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 28 163 | 19 097 |
| 12. Mali Nyingine | 5 143 | 5 015 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 846 | 918 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **43 286** | **38 763** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18. Amana za Wateja | 24 036 | 18 525 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 819 | 941 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 145 | - |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 341 | - |
| 27. Dhima Nyingine | 1 488 | 1 892 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **26 829** | **21 358** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **16 457** | **17 405** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30 912 | 30 912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (18 507) | (14 445) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (948) | (4 062) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji (Mtaji tangulizi) | 5 000 | 5 000 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **16 457** | **17 405** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 273 | 389 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (330) | (330) |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 38% | 45% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.0% | 1.7% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 116% | 103% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 64% | 50% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 77% | 71% |
| - Ongezeko la Amana | 30% | 67% |
| - Ongezeko la Mali | 12% | 29% |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 31-Mach-2021 | Robo ya mwaka Linganishi 31-Mach-2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mach-2021 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Mach-2020 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 1 012 | 673 | 1 012 | 673 |
| 2. Gharama za Riba | 343 | 123 | 343 | 123 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **669** | **550** | **669** | **550** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | (1) | - | (1) |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 91 | 60 | 92 | 60 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | - | 3 | 0 | 3 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 91 | 55 | 91 | 55 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | 2 | - | 2 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 1 708 | 1 563 | 1 709 | 1 563 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 732 | 662 | 732 | 662 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 976 | 901 | 976 | 901 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **(948)** | **(952)** | **(948)** | **(952)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **(948)** | **(952)** | **(948)** | **(952)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(948)** | **(952)** | **(948)** | **(952)** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 54 | 60 | 54 | 60 |
| 14. Mapato kwa Hisa | -15 | -15 | -15 | -15 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *-2%* | *-3%* | *-2%* | *-3%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *-6%* | *-6%* | *-6%* | *-6%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *225%* | *256%* | *225%* | *256%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *2%* | *3%* | *2%* | *3%* |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 31-Mach-2021 | Robo Mwaka iliyopita 31-Des-2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mach-2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Mach-2020 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | (948) | (969) | (948) | (952) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 346 | 385 | 346 | 295 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (5 766) | (7 720) | (5 766) | 388 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 5 511 | 2 850 | 5 511 | (547) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (242) | 160 | (242) | 313 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (802) | (717) | (802) | 519 |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | (281) | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(1 902)** | **(6 292)** | **(1 902)** | **16** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | (40) | - | (12) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **-** | **(40)** | **-** | **(12)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo (Mtaji tangulizi) | - | 5 410 | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **-** | **5 410** | **-** | **-** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - | - | - |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | (1 902) | (922) | (1 902) | 4 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 4 859 | 5 781 | 4 485 | 1 557 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 2 958 | 4 859 | 2 583 | 1 561 |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2021 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Mtaji tangulizi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30 912 | (18 507) | - | - | 12 405 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (948) | - | - | (948) |
| Mtaji tangulizi | - | - | - | 5 000 | 5 000 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30 912** | **(19 455)** | **-** | **5 000** | **16 457** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30 912 | (14 445) | - | - | 16 467 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (4 062) | - | - | (4 062) |
| Mtaji tangulizi | - | - | - | 5 000 | 5 000 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30 912** | **(18 507)** | **-** | **5 000** | **17 405** |

### BAADHI YA MAELEZO
### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2021

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha za robo, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | …………………… (Imesainiwa) | 22 Aprili 2021 |
| Selemani Kijori (Mkuu wa Fedha) | …………………… (Imesainiwa) | 22 Aprili 2021 |
| Patrick Mashalla (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | …………………… (Imesainiwa) | 22 Aprili 2021 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani | …………………… (Imesainiwa) | 22 Aprili 2021 |
| 2/ Celestin Muganga | …………………… (Imesainiwa) | 22 Aprili 2021 |

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES MADE UNDER REGULATION 11

| S/N. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **Current Accounts** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 50 000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 7 500 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 2,500 for amounts less than 5Mil otherwise 0.1% max TZS 100,000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | TZS 1 300 |
| | (e) ATM mini statement | TZS 300 |
| | (f) Interim statement per page | TZS 1 500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 0 |
| | (h) Cheque book | TZS 500 per leaf |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 100 000 |
| | (j) Special clearance | n/a |
| | (k) Counter cheque | TZS 6 000 |
| | (l) Stop payment | TZS 40 000 |
| | (m) Standing order (Same bank) | Free |
| | (n) Balance enquiry | TZS 300 |
| | (o) New ATM card issuance | TZS 10 000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | TZS 10 000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 20% |
| | (r) Unarranged overdraft | 20% |
| | (s) Interbank transfer | TZS 10 000 |
| | (t) Bill payments through ATM | n/a |
| | (u) Deposit fee | 0 |
| | (v) Other (please specify) | n/a |
| 2 | **Savings Accounts (Disclose for product specific types)** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 5 000 |
| | (b) Monthly service fee | TZS 1 400 |
| | (c) Interim statement | TZS 1 500 |
| | (d) Account closure | TZS 20 000 |
| 3 | **Electronic Banking** | |
| | (a) Internet banking monthly fee | n/a |
| | (b) Internet transfers | n/a |
| | (c) SMS banking | TZS 1700 |
| | (d) Other | n/a |
| 4 | **Foreign Exchange Transaction** | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the | n/a |
| | (b) Purchase of foreign cheque | n/a |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | n/a |
| | (d) Telegraphic transfer | n/a |
| | (e) Telex/SWIFT | n/a |
| | (f) Tranfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | 0 |
| 5 | **Personal Loans** | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | 1.77% p.a |
| | (i) Personal loans | 16% |
| | (ii) Overdrafts | 20% |
| | (iii) Mortgage finance | n/a |
| | (iv) Asset finance | n/a |
| | (b) Unpaid loan instalment | 20% |
| | (d) Valuation fees | n/a |
| | (e) Other | n/a |

**Deposit Rates**


| Fixed Deposit - TZS | 3 Months | 6 Months | 12 Months |
|---|---|---|---|
| 1 - 2 Mln | 1.5% | 2.0% | 2.5% |
| 2 - 10Mln | 2.0% | 2.5% | 3.0% |
| 10 - 50 Mln | 2.5% | 3.0% | 3.5% |
| 50 - 100 Mln | 3.0% | 3.5% | 4.0% |
| 100 - 300 Mln | 3.5% | 4.0% | 4.5% |
| 300 - 500 Mln | 4.0% | 4.5% | 5.0% |
| 500m - 1Bln | 4.5% | 5.0% | 5.5% |
| Above 1 Bln | Contact Treasury | | |
| **Savings Account - TZS** | **Accrue on Daily Cleared balance paid Monthly** | | |
| 0- 50k | 0.5% | | |
| 50k - 1mln | 1.0% | | |
| 1 - 10mln | 1.5% | | |
| 10 - 100mln | 2.0% | | |
| Over 1mln | 2.5% | | |

**Base Lending Rates**

| | Loan Type | Base rate | |
|---|---|---|---|
| 1 | Short term (up to 1year) | 19.5% | +/-4.5% |
| 2 | Medium term (2-4 years) | 21.5% | +/-1.5% |
| 4 | Term loans (over 5 years) | 19.0% | +/-4.0% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Richard L. Makungwa | Chief Executive Officer | | 22 April 2021 |
| 2 | Leticia Ndongole | Ag. Head of Business Development & Marketing | | 22 April 2021 |
| 3 | Selemani Kijori | Head of Finance | | 22 April 2021 |




**Head Office**
**Mlimani Tower - Mezzanine Floor,**
**Sam Nujoma Road**
**Phone: 022-2772954/7**
**email: info@mcb.co.tz**
**Customer Care No.: 0629331151|0629331755|080 0750033**

**Mlimani Branch**
**Mlimani Tower - Ground Floor**
**Sam Nujoma Road**
**P.O.Box 61002,**
**Dar es salaam**

**Samora Branch**
**Samora Avenue**
**Consolidated Holding Building Ground Floor**

**Regional Office - Morogoro**
**19, Plot E, Nkomo Street**
**Phone: +255 622 005 574**
**Morogoro**

**Regional Office - Mbeya**
**90, Plot L, Sokomatola Street**
**Phone: +255 766 903 575**
**Mbeya**

**Regional Office - Mwanza**
**18, Plot A, Kirumba Street**
**Phone: +55 788 138 238**
**Mwanza**

CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

TANGAZO

MAFUNZO YA UONGOZI NA MAADILI

Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), kinapenda kuwatangazia kuwa kutakuwa na Mafunzo maalumu ya Uongozi na Maadili yatakayofanyika kwa muda wa wiki moja. Lengo la Mafunzo haya ni kuwajengea uwezo washiriki katika stadi za Uongozi, Maadili na utawala bora na kuwajenga katika misingi imara ya Uongozi bora, uwajibikaji na uzalendo katika taasisi zao za Umma na binafsi kwa manufaa ya Taifa la Tanzania.

**Malengo mahususi ya Mafunzo**

i. Kujenga uelewa wa nadharia ya maadili na utawala bora na misingi ya utumiaji wa uelewa huo katika maeneo ya kazi.
ii. Kuboresha weledi wa washiriki katika kutatua migogoro na kufanya makubaliano ya kidiplomasia sehemu za kazi.
iii. Kuendeleza uwezo wa kufanya maamuzi kama viongozi na kupanua kiwango cha uelewa wa maadili na utawala bora kwa Washiriki.

**Walengwa**

Viongozi, Viongozi tarajali pamoja na Watumishi walio katika nyadhifa mbalimbali za kiuongozi katika taasisi za umma na binafsi.

**Muda wa Masomo**

Mafunzo yataendeshwa kwa muda wa wiki moja ambapo Mshiriki atachagua awamu moja kati ya nne kama ifuatavyo:

| Tarehe ya kuanza | Tarehe ya kumaliza | Mahali | Cheti kitakachotolewa |
|---|---|---|---|
| 3/5/2021 | 7/5/2021 | Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi na Maadili |
| 2/8/2021 | 6/8/2021 | MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi na Maadili |
| 23/8/2021 | 27/8/2021 | MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi na Maadili |
| 6/9/2021 | 10/9/2021 | MNMA, Kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam | Cheti cha Mafunzo ya Uongozi |

**Ada ya Mafunzo**

Gharama ya Mafunzo haya ni TZS 500,000/ ambayo italipwa kabla ya Mafunzo kuanza. Baada ya malipo, fedha haitaweza kurejeshwa.

**Jinsi ya kutuma maombi**

Maombi kwa ajili ya kuhudhuria Mafunzo haya yako wazi kuanzia sasa.

Mwombaji atatuma maombi yake kwa njia ya mtandao kwa kujaza fomu iliyokatika tovuti ya Chuo ambayo ni: www.mnma.ac.tz.

Mwisho wa kutuma maombi kwa ajili ya Mafunzo haya itakuwa ni wiki moja kabla ya tarehe husika ya kuanza kwa mafunzo.

**Mawasiliano**

**Kwa mawasiliano zaidi kuhusu programu hii maalumu ya Uongozi na Maadili unaweza kuwasiliana na Mratibu wa Mafunzo ya Uongozi na Maadili kupitia namba ya simu ya mkononi 255(22)2820041/47 au +255675337734: email: phillip.daninga@mnma.ac.tz au rector@mnma.ac.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkuu wa Chuo**
**Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

# Uvinza watengewa ekari 15,000 ardhi

**Na Mbaraka Kambona,** KIGOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameielekeza Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kutenga ekari 15,000 na kuzigawa kwa wananchi wa vijiji viwili vya Mpeta na Chakulu, wilayani Uvinza, mkoani Kigoma ili kutatua mgogoro wa ardhi wa muda mrefu baina ya wananchi hao na kampuni hiyo.

Ndaki alitoa maelekezo hayo juzi katika ziara yake wilayani humo kwa lengo kutatua mgogoro huo kutokana na wananchi wa vijiji hivyo kuvamia maeneo ya Ranchi ya Uvinza na kuishi kinyume na taratibu.

Akiongea na wananchi wa vijiji hivyo kwa nyakati tofauti, Waziri Ndaki alisema kuwa serikali imeamua kufikia uamuzi huo ili wananchi hao waweze kujikita katika shughuli za maendeleo na kuachana na migogoro ya kila siku ambayo haina tija.

"Hatupendi tuendelee na migogoro kwenye maeneo yetu, tunataka tumalize migogoro ili tuanze kufanya shughuli za maendeleo, kila mwananchi afanye shughuli yake bila bughudha yoyote," alisema Ndaki.

Alisema baada ya ugawaji wa maeneo hayo kukamilika Mkuu wa Wilaya ya Uvinza na timu yake watakwenda kufanya tathmini katika maeneo hayo na kuyafanyia mchakato wa kuyarasimisha ili kuwa kijiji au kitongoji.

Alisisitiza kuwa pamoja na wananchi hao kuvunja sheria, serikali imeangalia maslahi na ndio maana imeamua kutoa sehemu ya eneo katika ranchi hiyo ili wananchi hao waweze kuishi kwa utulivu na kuendelea na shughuli zao huku akiwaonya kuwa wasijaribu tena kuingia katika ranchi hiyo baada ya kugawa ekari hizo na atakayefanya hivyo anatafuta kesi.

"Ranchi ni eneo la kufugia mifugo na sio eneo la kuishi watu au kulima humo, atakayejaribu kuingia tena ananitafuta kesi, tumewapa maeneo hayo ili mkae humo, atakayetaka kufuga aje sisi tutampa eneo la kukodisha kwa bei ya serikali ili aweze kufuga kisasa, kulima malisho na kuongeza tija ya mifugo yake," alisisitiza Ndaki.

Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Mwanamvua Mrindoko baada ya kumshukuru Waziri Ndaki kwa uamuzi huo, aliwasisitiza wananchi hao kutoendelea kuvamia maeneo ya ranchi hiyo ili kuepuka migogoro na watumie maeneo hayo waliyopewa kujiletea maendeleo yao.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Chakulu, Mohamed Baswage, aliishukuru serikali kwa tamko hilo la kuwapa eneo wananchi wa kijiji hicho huku akisema uamuzi huo utawasaidia kusukuma maendeleo yao kwa pamoja wakishirikiana na serikali.

# TANCDA yapongeza serikali kuweka vipaumbele magonjwa yasiyoambukiza

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA), limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka vipaumbele vya serikali yake vita dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza (NCDs).

Pia, limempongeza kwa kutambua madhila yanayowapata wagonjwa wengi wa NCDs na kuahidi kuimarisha mifuko ya bima ya afya ili itoe bima kwa Watanzania wote, jambo ambalo limekuwa ni kilio cha shirikisho kwa muda mrefu sasa.

Akihutubia Bunge mjini Dodoma Aprili 22, Rais Samia alisema serikali yake itaweka nguvu katika kinga na tiba yakiwamo magonjwa yasiyoambukiza, ambayo yanasababisha vifo vingi na kugharimu serikali fedha nyingi.

Rais Samia pia alisema serikali itaimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na kuzipeleka kwenye hospitali za rufaa za mikoa.

Taarifa iliyotolewa na Katibu wa Shirikisho hilo, Prof Kaushik Ramaiya, ilisema shirikisho hilo linaipongeza serikali kwa kuahidi kuimarisha utoaji wa huduma za matibabu kwa wazee na kuweka mipango maalum kuhudumia makundi yenye magonjwa adimu.

Vile vile, kuahidi kuimarisha Mifuko ya Taifa ya Bima ya Afya ili kufikia lengo la Bima ya Afya kwa wote na kutoa takwimu kuwa kwa sasa ni watu 8,224,271 sawa na asilimia 14 pekee ya Watanzania ndio wanaotumia Bima ya Afya.

"TANCDA imefarijika sana na mkakati huu wa Serikali Awamu ya Sita kwa kuzingatia kwamba magonjwa yasiyoambukiza yanaongezeka kwa kasi na hata kuwaathiri watu wenye umri mdogo, wakiwamo watoto," alisema Prof. Ramaiya katika taarifa yake.

Alisema tafiti za kisayansi zinaonesha kuwa mwaka 2016, watu milioni 42, sawa na asilimia 71 ya vifo vyote duniani, walipoteza maisha kutokana na magonjwa yasiyoambukiza na pia asilimia 75 ya vifo vyote vinavyohusu watu wenye umri kati ya miaka 30 hadi 70

Magonjwa yasiyoambukiza ni magonjwa yasiyo na vimelea vinavyoweza kusambazwa kutoka kwa wanaougua kwenda kwa wengine. Mfano magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, saratani, magonjwa sugu ya njia ya hewa, kisukari, kuoza meno, magonjwa ya akili na mengineyo ya kurithi kama vile siko seli.

Kwa Tanzania inakadiriwa ya kuwa magonjwa hayo yanasababisha asilimia 27 ya vifo vyote na utafiti wa mwaka 2012 unaonyesha kuwa kwa kila watu 100 wenye umri kuanzia miaka 25 na kuendelea; tisa wana kisukari, 26 wana shinikizo la damu, 25 wana mafuta yaliyozidi kwenye damu na 34 wana uzito ulizidi.

Zipo sababu mbalimbali zinazosababisha magonjwa haya zikiwamo za kutozingatia mitindo bora wa maisha kama vile ulaji usiofaa, kutoshughulisha mwili, matumizi ya vilevi kupindukia na matumizi ya tumbaku

"TANCDA inajikita zaidi katika kuelimisha jamii kufahamu magonjwa haya kwa sababu utafiti wetu unaonesha kuwa kila mtu akifahamu kinagaubaga magonjwa haya itakuwa rahisi kuyaepuka," alisema.

Vile vile, TANCDA inaelimisha na kuhimiza wale ambao tayari wanaugua magonjwa haya kuzingatia kanuni wanazoelekezwa na wataalamu wa afya ili kuyadhibiti na kuwafanya waishi maisha marefu.

# Waziri aipa siri CTI kutatua changamoto

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi (Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, ameitaka jumiya ya wafanyabiashara nchini inapoandaa vikao vyake na wizara mbalimbali ni vyema vikafanyika chini ya utaratibu na Baraza la Taifa la Biashara(TNBC) ili kuleta wepesi wa ufuatiliaji wa changamoto na mapendekezo kufika katika ngazi husika.

Amesema hatua hiyo itasaidia kuboresha mazingira ya biashara nchini.

Waziri Mwambe alizungumza hayo alipokuwa akifungua mkutano wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), uliolenga kujadili changamoto zinazoikabili sekta ya viwanda na kuja na mapendekezo yatakayosaidia kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

"Ni muhimu mikutano kama hii ishirikishe TNBC ili tija iweze kupatikana ya kuandaa mikutano kwani mapendekezo na changamoto zitakazotolewa vitawasilishwa katika kila wizara kwa umuhimu wake na kutafutiwa ufumbuzi," alisema Waziri Mwambe.

Aliongezea kuwa inaposhirikishwa TNBC inakuwa ni kiunganishi kati ya sekta binafsi na serikali kwani jukumu lake kubwa ni kusimamisha majadiliano na kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia uwekezaji nchini.

"Serikali imekusudia kufanya mapitio upya ya sheria na sera ya uwekezaji ili kwenda sambamba na mazingira ya sasa jambo ambalo litaongeza kwa wafanyabiashara na wawekezaji kwa kuyaangalia maeneo ambayo yamekuwa changamoto kubwa hapa nchini," alisema Waziri Mwambe.

Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alisema muundo mpya wa Baraza umelenga kufanya vikao kuanzia ngazi ya wilaya na mkoa ili kupata ufumbuzi wa changamoto za ufanyaji biashara na uwekezaji.

Dk. Wanga aliwahakikishia CTI kuwa baraza litaendelea kufanya majadiliano na sekta binafsi kwa kuwa ndicho chombo maalum kinachounganisha serikali na sekta binafsi.




Vijana wakivuta mnyororo kwaajili ya kuvuta lori la mafuta ambalo liligongana na lori lililobeba shehena ya mkaa na kukaribia kutumbukia kwenye mteremko wa mlima Kitonga mkoani Iringa mwishoni mwa wiki **PICHA JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wakulima shairi, zabibu, na mtama wapata fursa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amesema wizara yake imejipanga kuongeza uzalishaji wa mazao ya shairi, zabibu na mtama kutokana na uhitaji wake kuwa mkubwa kama malighafi muhimu katika uzalishaji wa bia.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma mwishoni mwa wiki baada ya kufanya mazungumzo na uongozi wa kampuni ya kutengeneza, kuuza na kusambaza bia (TBL), Waziri Mkenda alisema sehemu kubwa mazungumzo yao yalilenga kuongeza uzalishaji wa shairi, zabibu na mtama ili kuhudumia kiwanda kinachojengwa mkoani hapa.

"TBL wamekuwa wakizalisha bia kutokana na shairi ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikiagizwa kutoka nje ya nchi, tumekutana kuona namna bora ya kuongeza uzalishaji wa shairi nchini ambayo imekuwa ikilimwa mikoa ya kusini na kaskazini," alisema.

Waziri Mkenda alitumia nafasi hiyo kutoa wito kwa wakulima kutumia fursa ya uwapo wa kiwanda hicho kuongeza uzalishaji wa zao la shairi kwani soko la uhakika litapatikana.

"Nitoe wito kwa wakulima wa shairi, mtama pamoja na zabibu ambayo ni malighafi muhimu kwa uzalishaji wa mvinyo, kuongeza uzalishaji kwani uhitaji wa mazao hayo ni mkubwa kwa viwanda vya kutengeneza bia," alisema na kuongeza kuwa wataalamu wa ugavi watakuwa mstari wa mbele kuwaongoza wakulima.

Alisema Wizara yake itawatumia wataalamu kuhakikisha uzalishaji wa malighafi hizo unaongezeka ili kumnufaisha mkulima kwa kumpatia soko la uhakika na viwanda kupata malighafi za kutosha.

"Mkakati tulionao kama wizara ni kutumia watafiti, upimaji wa afya ya udongo pamoja na kuhimiza matumizi ya mbegu bora ili kuongeza uzalishaji wa chakula kwa mazao ya mtama pamoja na malighafi ambazo zimekuwa zikihitajika kwenye viwanda vyetu vya ndani," alisema Waziri Mkenda.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

## TAARIFA KWA UMMA

### KUONGEZWA KWA MUDA WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WANUFAIKA WA MWISHO (BENEFICIAL OWNERS)

**Dar es Salaam, Aprili 08, 2021**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) unapenda kuwataarifu Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kwamba Waziri wa Viwanda na Biashara, kupitia Tangazo la Serikali Na. 189 la tarehe 12 Februari 2021 ameongeza muda wa miezi kumi na miwili (12) kuanzia tarehe 1 Januari, 2021 kwa ajili kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) kwa kampuni zilizosajiliwa kabla ya tarehe 1 Julai, 2020.

Takwa hili la kuwasilisha taarifa tajwa ni matokeo ya marekebisho ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 (Finance Act, 2020) kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners).

Aidha Kifungu cha 459A cha marekebisho hayo, ambacho kilizitaka Kampuni zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 kabla ya tarehe 1 Julai, 2020 kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) ndani ya kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Julai, 2020.

BRELA kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Kanuni za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) zitakazoweka bayana utaratibu wa kukusanya na kuhifadhi taarifa hizi.

BRELA inawataka Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kutumia vizuri muda huu wa nyongeza kuwasilisha taarifa husika mapema na sio kusubiri muda wa mwisho ili kuepusha usumbufu wa namna yeyote unaoweza kujitokeza.

**Imetolewa na**
**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**

Jengo la Ushirka, Mtaa wa Lumumba, S.L.P. 9393, Dar Es Salaam, Simu: +255-22-2181344, 2180113, 2180141, 2212800, Nukushi: +255-22-2180371, barua pepe: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz , Tovuti: www.brela.go.tz

# Waziri apigia debe soko mahindi Congo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, amewasihi wadau katika sekta ya kilimo kuwasaidia wakulima kuzalisha mahindi mengi ili wanufaike na soko zuri la zao hilo katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Akizungumza jijini hapa baada ya kukutana na wataalamu wa mbolea, Waziri Mkenda alisema wakulima wa mahindi wa Tanzania wakilima mahindi kwa bidii na kwa ufanisi na kuzalisha ziada, watanufaika na soko zuri la zao hilo Kongo.

Aliwambia waandishi wa habari kwamba sekata ya kilimo ina fursa tele kwa wakulima za kujiongezea kipato kwa kuwa kuna mahitaji makubwa ya mazao ya chakula katika nchi zinazoizunguka Tanzania, hasa mahindi.

"Nachukua fursa hii kuwambusha wakulima wetu kuwa kuna fursa nyingi za mazao ya chakula. Kwa mfano, huko Congo kuna mahitaji mkubwa ya mahindi. Kwa hiyo hii ni fursa ya kuchangamkia ambayo inaweza kuwongezea kipato wakulima wetu," alieleza.

Tanzania na DRC zina uhusiano mzuri wa biashara na wa muda mrefu. DRC hununua mazao ya chakula hasa nafaka, mazao ya aina ya jamii ya kunde na samaki kutoka Tanzania hasa mikoa ya nyanda za juu ya kusini mwa Tanzania. Mikoa inayouza mazao Kongo ni Mbeya, Songwe, Katavi, Rukwa na Kigoma.

Ili kurahisisha na kuimarisha biashara kati ya nchi mbili, serikali imewekeza bilioni 11 katika kupanua na kuboresha bandari za Kabwe na Kasanga na Kipili na gati ya Kirando. gati ya Kirando hutumika kusafirisha bidhaa kutoka Tanzania na kupokelewa katika Bandari ya Nkolusha ya DRC.

Mbali ya kuowaomba wadau kuwasaidia wakulima, Profesa Mkenda aliwasihi wakulima kubadili mtazamo wao juu ya kilimo ili uzalishaji katika eneo wanalolima uongezeke. Ametoa mfano wa mkulima wa Afrika ya Kusini, ambaye amesema kwa sasa anapata maguni 40 katika eka wakati mkulima wa Songwe anapata magunia 12.

Waziri alisema moja ya vipaumbele vya serikali ya awamu ya sita ni kutumia kilimo kupambana na umaskini kwa kuongeza tija katika sekta hiyo. Amefafanua kuwa sekta ya kilimo inachangia chini ya theluthi moja katika pato la taifa, kwa sababu ya uzalishaji mdogo wakati sekta ya utalii inachangia takariban asilimia 17.5.



Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Elias Kwandikwa, akizungumza na wananchi wa Kata ya Nyamilangano, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wakati akisikiliza kero za wananchi na kuwapongeza kwa kumchangua kwa kishindo katika uchaguzi mkuu uliopita jana. **PICHA; SHABAN NJIA.**

# CRB yasajili makandarasi wapya 907

**Na Joseph Mwendapole,** MBEYA

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB) imesema kwa mwaka 2020 pekee imesajili makandarasi wapya 907 hivyo kufikia makandarasi 11,749 nchini.

Hayo yalisemwa na Msajili wa Bodi hiyo, Rhoben Nkori, kwenye mafunzo ya siku mbili kwa makandasi 300 wazawa yaliyofanyika nyanda za juu kusini Mbeya.

Alisema mbali na kusajili makandarasi, CRB iliendesha kozi sita na kusajili miradi 3,179 yenye thamani ya Sh. trilioni 3.8 ambayo ilifanywa na makandarasi wa ndani na wa nje.

Alisema mwaka 2020 bodi ilikagua miradi 3,364 ambapo miradi 2,430 ambayo ni asilimia 72 haikukutwa na kasoro wakati miradi 934 ilikuwa na kasoro mbalimbali ikiwamo kutozingatia usalama kazini.

Alisema kwenye ukaguzi huo walibaini baadhi ya makandarasi kufanyakazi zilizo zaidi ya madaraja yao na miradi hiyo kutosajiliwa na bodi kama inavyotakiwa.

Alisema CRB imeendelea kuimarisha mfuko wa kusaidia makandarasi (Contractors Assistance Fund- CAF) kwa kuwadhamini wazalendo benki ya CRDB ili wapewe dhamana kwaajili ya zabuni na malipo ya awali yaani advance payment.

Alisema mwaka 2020 bodi ilifanikiwa kufanya majadiliano na benki ya CRDB na kufikia makubaliano ya kudhamini makandarasi wa ndani wa madaraja yote badala ya makandarasi wadogo na wakati .

Nkori alisema bodi ilihakikisha kiwango cha dhamana kinaongezeka kutoka Sh milioni 50 hadi milioni 100 ingawa alisema kiasi hicho bado ni kidogo kulinganisha na mahitaji halisi ya makandarasi .

Nkori alisema mikutano hiyo ya mashauriano imekuwa muhimu kwani bodi imekuwa ikikutana na waajiri wakuu na wasimamizi wa sera na kujadiliana na kufanya maboresho kwenye upungufu.

Alisema mikutano hiyo ambayo hufanyika kila mwaka imekuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya makandarasi nchini kwani wengi wameboresha kazi zao.

Nkori alitaja baadhi ya maazimio ya makandarasi hao kuwa ni kuitaka Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) iweke utaratibu mzuri wa kuwaelimisha makandarasi kuhusu masuala ya kodi na kutoza kodi halisikulingana na biashara ya ukandarasi.

Alisema makandarasi wameomba malipo yao yafanyike kwa wakati pale yanapocheleweshwa yalipwe kwa riba kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma.

Nkori alisema makandarasi wamekubaliana kwa pamoja wajiepushe na vitendo vya rushwa na wanaposhawishiwa na watoa kazi watoe taarifa kwa mamlaka husika.

# Serikali yaombwa mtaala wa uhifadhi wa mazingira

**Na Ashton Balaigwa,** KIBAHA

BALOZI wa Mazingira nchini ambaye ni Mhitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Zuhura Ahamad, ameiomba serikali kuchukua hatua mahsusi za kuingiza kwenye mitaala masomo ya Uhifadhi wa Mazingira na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi.

Lengo ni kuwafanya wanafunzi waanze kujifunza tangu hatua za awali pamoja na kuachana kabisa na nishati hatarishi zinazoathiri mazingira.

Amesema hatua hiyo itaweza kuiokoa Tanzania kutoingia katika hatari ya moja ya nchi duniani ambazo zitakuwa sio salama kwa kuishi katika miaka ijayo kutokana na kuangamia na kutoweka kwa bainowai na viumbe hai kwa sababu za uharibifu wa mazingira.

Balozi huyo wa mazingira ambaye ni mwakilishi wa vijana, alisema hayo wakati wa maadhimisho ya siku Mama Dunia (Mother Earth Day) yaliyofanyika kwenye Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI Kibaha) yaliyoshilikisha wanafunzi kutoka shule mbalimbali za Mkoa wa Pwani ambayo yalikuwa na kauli mbiu ya Kimataifa 'Hifadhi Dunia yetu".

Akiwasilisha ujumbe huo, alisema, tayari kumeshaanza kujitokeza kwa athari za uharibifu wa mazingira nchini na kusababisha ukame, mafuriko, magonjwa ya mlipuko wa msongo wa mawazo kutokana na joto au baridi ya kupitiliza, hivyo ni vyema serikali sasa ikachukua hatua za makusudi za kuhifadhi na kutunza maliasili kwa ajili ya kuepusha kutokea kwa madhara hayo.

Kaimu Mkurugenzi wa TARI Kibaha, Dk. Heldelitha Msita, alisema katika kuunga mkono, wameandaa kampeni ya kupanda miti 1,000 ya matunda na vivuli katika maeneo yanayozunguka taasisi hiyo na tayari mpaka sasa wameshapanda jumla ya miti hiyo 500 ili kuhifadhi Mama Dunia.


Alisema kampeni hiyo inalenga kutoa elimu kwa wanafunzi na kuikumbusha jamii kuhusiana na faida za uhifadhi wa mazingira kwa vizazi vilivyopo na vijavyo, kwa kuwa gharama za kurudisha mazingira ni kubwa kuliko za kuhifadhi mazingira .

" Hakuna kati yetu ambaye hajawai kukumbwa na changamoto mbalimbali zinazotokana na uharibifu wa mazingira kama vile ukame unaopelekea ukosefu wa chakula, mafuriko yanayopelekea vifo, uharibifu na ukosefu wa makazi , magonjwa ya milipuko kama kipindupindu na ongezeko la joto, " alisema Dk. Msita.

Dk. Msita aliwataka wananchi, vyombo vya habari, taasisi zote za serikali na Asasi za kiraia kuweka mikakati mbalimbali ya kuhifadhi mazingira pamoja na vyanzo vya maji, uvunaji holela wa misitu na ufugaji usio endelevu pamoja na kupanda miti mingi wakati wa msimu wa mvua ili kujihami na kuenea kwa hali ya jangwa na mabadiliko ya tabianchi.

Naye Ofisa Maliasili mkoa wa Pwani, Felix Shayo, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa mkoa huo, Mhanidisi Evarist Ndikilo, alisema anatambua zipo changamoto za utekelezaji wa zoezi la utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika mkoa huo ikiwamo kukosekana kwa elimu ya kutosha ya mazingira,upatikanaji wa nishati mbadala ya kupikia, uchafuzi wa vyanzo vya maji na matumizi ya kemikali zisizo sahihi kwenye kilimo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 27, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

## Ajabu Watanzania kuishi kinadharia



Ukurasa 12

ILO inavyokomesha unyanyasaji, ukatili



Ukurasa 13

Udhaifu huu ungetazamwa mimba shuleni zingepungua

ELIMU

**NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR**

WADHALILISHAJI WAMEKOMA

# 160 waburuzwa kortini

FEBRUARI mwaka huu, Wazanzibari walishuhudia kuanzishwa mahakama maalum ya kesi za udhalilishaji ambayo imenza kwa mafanikio, huku kasi ya kufungua kesi ikiongezeka.

Takwimu zinaonyesha kuwa hadi sasa mashauri zaidi ya 160 yamefikishwa mahakamani, kote Unguja na Pemba.

Kati ya kesi hizo, mbili zimesikilizwa na hukumu kutolewa huku nyingine zikiendelea , anasema Mrajisi wa Mahakama Kuu Zanzibar, Muhammed Ali Muhammed.

Anafafanua kuwa kesi hizo 160, zimefikishwa katika mahakama za Unguja na Pemba katika kipindi cha mwezi mmoja.

Anaeleza kuwa kesi zilizofunguliwa ni pamoja na 94 katika Mahakama ya Vuga, Mahonda zipo 26, Mahakama ya Mwera ni 21 na katika Mahakama ya Chake Chake Kusini Pemba kuna kesi 10 wakati Wete Kaskazini Pemba zipo mbili.

Anaeleza kuwa kuanzishwa mahakama maalum ya kushughulikia kesi za udhalilishaji Zanzibar, kumewashajihisha (kuhamasisha) watu wengi kuongeza juhudi za kupambana na udhalishaji, hasa wa watoto.

Mwamko huo unaelekea kuleta matumaini ya kusaidia kupunguza au kutokomeza vitendo hivyo ambavyo kasi yake ilikuwa kubwa Unguja na Pemba katika miaka ya karibuni.

Anakumbusha kuwa mahakama hiyo ilianzishwa rasmi Februari, mwaka huu baada ya Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, kuagiza kuundwa kwa chombo hicho, kufuatia malalamiko na matukio ya kushamiri vitendo vya udhalilishaji.

### CHANGAMOTO ZINAZOIBUKA

Uhaba wa mahakimu unatajwa na Muhammed kuwa ni miongoni mwa changamoto zilizijitokeza katika kuunda mahakama maalum.

Lakini anasema inapata utatuzi baada ya serikali kutoa kibali cha kuajiri mahakimu wapya ili kuendesha shughuli za mahakama hiyo kwa ufanisi.

"Wakati wote kuanzia sasa tutawapata na kazi yao itakuwa kushughulikia kesi za udhalilishaji pekee na hawatahusika na nyingine kama wizi wa kuku au matunda,"anasema Mrajisi.

Anathibitisha kuwa kesi za udhalilishaji zipo nyingi na kwamba utaratibu uliowekwa unaagiza kesi isichukue zaidi ya siku 90 kabla ya kupatiwa uamuzi.

Anataja tatizo la majengo kuwa ni changamoto nyingine na kwamba Mahakama inatumia majengo ya Mahakama ya Mikoa Unguja na Pemba.

### KUPATA MASHAHIDI

Muhammed anataja usumbufu katika kupata ushahidi wa kesi hizo, hasa wanapoitwa mahakamani.

"Wengi hukataa kufika kwa kutoa sababu mbalimbali, ikiwamo ya muhali (jamaa kuoneana aibu). Lakini kuwapo kwa mahakama maalum kutasaidia kupunguza tatizo kwa sababu mahakama hii inao uwezo wa kuwapa adhabu wanaokataa kutoa ushahidi." Anasema



Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Mwinyi Talib Haji. **PICHA: MTANDAO**

Anaitaka jamii kutoa ushirikiano wanapoitwa kutoa ushahidi ili kesi hizo kupatiwa hukumu zinazostahiki kwa sababu bila watuhumiwa hawatatiwa hatiani.

Anasema kuna kibano kwa mashahidi wanaokataa kufika mahamani na hakitakuwa kwa watakaokataa pekee bali pia kwa hakimu ambaye hatafika mahakamani bila sababu za msingi.

Anawataka mahakimu kuelewa kwamba wanawajibika kufika mapema mahakamani na kuonya kwamba atakayeshindwa kuwajibika atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Mrajisi anasema kuongezeka kwa kesi hizo ni kuporomoka kwa maadili, matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii, tamaa kwa watoto na malezi duni ndani ya baadhi ya familia.

Anashauri vyombo vinavyoshughulika na kesi hizo kukutana mara kwa mara ili kupata njia mwafaka za kushughulikia tatizo hili. Anawakumbusha mahakimu kutumia sheria kama zinavyoelekeza katika kutoa hukumu na wasifumbe macho wala kutetereka mikono katika kutumia kalamu zao kwa misingi ya sheria na haki.

"Ninaamini kufanya hivyo jamii itaweza kurejesha imani kwa mahakama na serikali na hatimaye kupatikana mwarobaini wa udhalilishaji,"

Mrajisi anatoa tahadhari kwa jamii isiwe chanzo cha uonevu kwa kubambikiza kesi kwa sababu kuna baadhi ya kesi za aina hiyo zinazolenga kuwakomoa wengine.

### MAELEZO YA DPP

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar (DPP) inasema inaazimia na imejipanga kuendesha kiweledi kesi za udhalilishaji katika mahakama maalum. "Mpango huu unajumuisha kutoa mafunzo kwa wanasheria na kuajiri wapya ambao watashughulikia kesi hizo, " anasema Mkuu wa Utafiti na Ushauri wa Ofisi ya DPP, Ramadhan Abdalla Nassib.

Anaongeza kuwa kati ya wanasheria 10 wapya walioajiriwa, sita watafanya kazi Unguja na wanne Pemba.

Nassib anasema masuala ya udhalilishaji yanahitaji faragha hivyo ni vyema kupatikana majengo yatayokuwa na mazingira rafiki ya watu kujiona huru na kutojisikia aibu wanapotoa ushahidi.

" Kuanzisha kitu kipya ni gharama, lakini vitendea kazi na miundombinu ni muhimu na lazima ili mahakama hizi zifanye kazi kikamilifu,"anasema.

ELIMU

**NA GERALD KITABU**



# ILO inavyokomesha unyanyasaji, ukatili

DUNIA salama ya kazi haitapatikana bila umma unaohusisha waajiri, wafanyakazi na taifa linalosimamia masuala ya ajira kuufahamu mkataba 'C 190' wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) unaotoa tafsiri na maana ya ukatili na unyanyasaji kazini.

Ili kuiwezesha jamii kuufahamu, vyombo vya habari vinapewa jukumu la kuelimisha na kukuza uelewa wa mkataba huo ambao unatoa tafsiri na maana ya ukatili na unyanyasaji kazini, unazipa nchi wanachama kuweka tafsiri zaidi.

Wakili Annery Nahum (pichani), akifafanua zaidi, anasema mkataba huo unawahusu wafanyakazi wa sekta zote, aidha unawalenga pia wanaotafuta kazi, wanaohudhuria mafunzo kwa vitendo, wanaoomba, walioachishwa kazi, wanaojitolea kazini na waajiri.

Anayasema hayo wakati wa mafunzo kwa wanahabari ili kuwajengea uwezo kuhusu mkataba huo, yanayoandaliwa na shirika la Actionaid.

> “Waandishi ni wadau muhimu kwa sababu kwa kutumia taaluma na weledi wao wanaweza kuwafikia watu wengi zaidi kwa wakati mwafaka.

**CHIMBUKO C 190**

Nahum anasema mchakato ulianza mwaka 2015 kwa lengo la kufuta kilio cha dunia kuhusu ukatili na unyanyasanyi mahali pa kazi. “Mkataba huu unatoa mwongozo na nafasi ya kutengeneza ajira na kazi zinazoheshimu utu na kuwa huru mbali na ukatili na unyanyasaji au viashiria vyake kuliko ambavyo imewahi kuelezwa au kufafanuliwa katika mkataba mwingine wa kimataifa,” anasema.

Anaongeza kuwa mkataba huo unatambua kuwa unyanyasaji na ukatili ni ukiukwaji wa haki za binadamu, kwa hiyo vyombo vya habari vina wajibu wa kuelimisha jamii ili ufahamike.

Anasema unataja maeneo ambayo ukatili na unyanyasaji unaweza kutoka kwenye safari za kikazi, vifaa vya mawasiliano, eneo la malazi unayopewa na mwajiri wako na unapoelekea au kutoka kazini .

Akizungumzia nguzo za mkataba huo, Wakili Nahum anasema ni lazima kila mtu aheshimu kazi ya mwingine, aidha asimamie usalama na ulinzi wa haki za wengine.

Nahumu anataja kanuni nyingine kuwa ni kutambua haki za wengine kazini dhidi ya ukatili na unyanyasaji.

“Kwa mara ya kwanza jumuiya ya kimataifa imefanya uamuzi na kuchukua hatua madhubuti za kimataifa kuwa haki ya kazi na ajira inakuwa huru na ukatili na unyanyasaji kupitia mkataba wa kimataifa Na. C 190.”

Pia unaweka mfumo wa kuzuia na kueleza ukatili, unyanyasaji na ukatili kijinsia kwa namna jumuishi.

**MAFANIKIO YA C 190**

Nahumu anasema ni mkataba unaohitajika kwa vile ukatili na unyanyasaji unaathiri nchi, taasisi, taaluma, mipangilio ya kazi, utu na unakwenda kinyume na kazi za staha na haki ya jamii.

Anasema, haki ya jamii ina dhumuni la kutenda haki baina ya madaraja yaliyopo katika jamii na siyo watu.

Anaongeza kuwa, haki ya jamii haitafikiwa iwapo wanaofanya kazi watanyimwa ujira au mshahara, hawataweza kujikimu wanapokuwa nje ya mfumo rasmi wa ajira, wanapokuwa hawana bima za uzeeni mara wanapostaafu na kwamba ili kufikia malengo hayo sharti kutunga sheria ambayo itaangazia hayo.

“Tafsiri hiyo haikutosha ndiyo maana ILO ikaongeza kusema ujira, pensheni, kuajiriwa pekee siyo kipimo tosha kufikia haki ya jamii. Ikaongeza, kuondoa ukatili na unyanyasaji mahali pa kazi. Haki ya Jamii inaangazia usawa kupita haki ya mtu. Hivyo lengo la sheria za ajira ni kuhakikisha maendeleo ya uchumi, haki ya jamii.

Mengine ni utulivu na demokrasia mahali pa kazi, ikiwa ni pamoja na kuwapo mifumo ya usuluhishi wa migogoro.

**NANI ANALINDWA NA C190**

Mkataba unahusisha ulinzi kwa wote wanaohusika na kazi au ajira, awe mwenye mkataba wa ajira au hana, wanaojitolea, walio kwenye mafunzo kwa vitendo na wanaosaka ajira, waajiri wa sekta binafsi na ya umma au sekta isiyo rasmi mjini au vijijini.

Kuna pia makundi yaliyo katika hatari ambayo yanaweza kufanyiwa ukatili na kunyanyaswa, mfano, watumishi wa afya, usafirishaji, elimu, wafanyakazi wa ndani, , wanaofanya kazi usiku au maeneo yaliyojitenga mfano wanahabari, wanawake, ajira kwa watoto, walioajiriwa sekta isiyo rasmi pamoja na wanaoishi na ulemavu.

**UTEKELEZAJI**

Wakili Nahumu anasema mkataba huu utaanza kutekelezwa miezi 12 baada ya nchi mbili wanachama kuweka saini. Hivyo ifikapo Juni 25, 2021 utaanza kutekelezwa kwa vile nchi 3 zimeshatia saini.

Meneja Miradi ya Wanawake wa Actionaid, Amne Manangwa, anasema ni muhimu vyombo vya habari vikauelewa vyema mkataba huu ili waandishi waweze kutumia taaluma zao kuielimisha jamii.

‘Waandishi ni wadau muhimu kwa sababu kwa kutumia taaluma na weledi wao wanaweza kuwafikia watu wengi zaidi kwa wakati mwafaka,” anasema.

Anasema katika mkataba huo ILO unagusa mambo ya msingi kama vile ustawi kwa wananchi wote na maisha yao na unahimiza kila mtu kulindwa anayefanya kazi bila kujali yuko kwenye sekta rasmi au isiyo rasmi.

“Ni matumaini yetu sote kuwa vyombo vya habari vitakuwa vinara kuelimisha umma na hivyo kuwafikia kwa wepesi wadau wote wa suala hili ili kwa pamoja wapunguze hata kumaliza unyanyasaji na ukatili mahali pa kazi na katika jamii zetu.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Udhaifu huu ungetazamwa mimba shuleni zingepungua

TATIZO la mimba na wanafunzi kushindwa kusoma iwe shule ya msingi au sekondari kutokana na ujauzito ni suala ambalo lingefaa kushughulikiwa kama hitaji 'spesheli' kwenye awamu ya sita.

Licha ya kukemewa mara kwa mara, swali ambalo halijajibiwa ni hili "ni nani anawajibika moja kwa moja kunapotokea ndoa au mimba za mabinti wakiwamo wanafunzi?

Mabinti wa msingi na sekondari wanapata mimba na tatizo hilo inaelekea kukua lakini hakuna ufumbuzi pengine kwa sababu hakuna anayebeba jukumu hilo, ili kuifikisha kesi mahakamani, baada ya polisi (Jamhuri) kuanza kazi yake.

Mwanafunzi anapopata mimba kuna kamati ya shule ya msingi, au bodi ya sekondari, walimu, ofisi ya ustawi wa jamii, wazazi , walezi na viongozi wa vijiji, kata, ofisa elimu kata na wakuu wa wilaya na mkoa.

Hivyo ni wakati wa kuuliza na kupata jibu hivi kati ya hao ni nani anayewajibika mwanzo hadi mwisho kusimamia kesi ya mimba ya wanafunzi?

Ni yupi anayeshirikiana na polisi kutafuta ushahidi, kuhakikisha watuhumiwa wamefikishwa mahakamani na kufuatilia mwenendo wa kesi kuanzia mwanzo hadi mwisho hukumu inapotolewa?

Kazi ya kufuatilia kesi hii inavyoelekea hubaki kuwa jukumu la mzazi au mlezi na wakati wadau wengine wamejiweka pembeni.

Hali ilivyo ni kama kesi hizo 'hazina mwenyewe' ndiyo maana zinaporipotiwa shuleni au mitaani, bado ni vigumu kuwakamata watuhumiwa.

Madai yamebakia kuwa hawafahamiki walipo au msichana anaeleza kuwa hamfahamu.



Waziri wa Elimu, Profesa Joyce Ndalichako. **PICHA: MTANDAO**

## VIPI KAMATI HII?

Kamati ya Shule ya Msingi ndicho chombo kinachosimamia maendeleo ya shule, hivyo unaporipotiwa ujauzito kwenye eneo hilo kamati ya shule humkabidhi mzazi au mlezi binti yake ili wamrudishe nyumbani.

Iwapo anasoma sekondari Bodi ya Shule ndiyo inayobariki na kumkabidhi binti huyo kwa wazazi na kumuondoa shuleni.

Utaratibu unaelekeza aondolewe shuleni na kamati ya shule inahusika kutimiza jukumu hilo.

Pengine ni wakati wa kuamua kuanzia sasa ni nani abebe jukumu la kufuatilia na kusimamia kesi za mimba za watoto shuleni pamoja na mitaani.

Ijulikane ni kamati au bodi ya shule, walimu wakuu, watendaji wa vijiji au maofisa elimu kata ili pamoja na polisi, wazazi walezi wasikosekane mahakamani.

Kuna haja ya kutoa maelekezo ili sheria na taratibu zifuatwe kupata watuhumiwa badala ya kuacha mambo yabaki kama yalivyo.

Pamoja na viongozi wa kijiji kupewa taarifa za mabinti kufukuzwa shule na Mtendaji wa Kijiji baada ya wasichana hao kuondolewa shuleni, kazi isiishie hapo wawe na jukumu la kuwa bega kwa bega na dola mahakamani.

## UPUNGUFU UONDOKE

Kwa zama hizi ambazo serikali inagharamia elimu ya msingi na sekondari kamati ya shule za msingi na bodi kwa sekondari kukaa vikao na kuidhinisha kufukuza wanafunzi wanaopewa ujauzito na kuwakabidhi kwa wazazi au walezi haupendezi.

Wajumbe hawa wawajibike kufuatilia na na kushughulikia kesi hizo kikamilifu kuhakikisha watuhumiwa wanapatikana, kushitakiwa na mimba za wanafunzi zinadhibitiwa.

Ukweli ni kwamba wasichana wanatimuliwa shuleni baada ya kuwa wajawazito, lakini watuhumiwa wanaowapa mimba wanatoroka .

Tatizo linakuwa kubwa kwa sababu hakuna jitihada zaidi zinazofanywa licha ya kesi kufikishwa polisi au mahakamani kwasababu wanakosekana watu au chombo cha kufuatilia na kuhakikisha mtuhumiwa anasakwa na kufikishwa kizimbani.

Kesi hizo hazina mwenyewe ndiyo sababu mabinti wakati mwingine wanaishia kuhangaika na wahusika hawafikishwi kwenye mkono wa sheria.

Iwapo mwanaume anatuhumiwa kumpa binti mimba haonekani wazazi , walezi , au kamati au bodi ya shule au viongozi wa kijiji wasakwe ikibidi washitakiwe ili nao wafanye kazi na kumnasa.

## ZIJE SHERIA NDOGO

Serikali ihamasishe na iwezeshe kuandaliwa sheria ndogo ndogo za manispaa au halmashauri na za vijiji zinazowezesha kuwapeleka rumande wahusika hao hadi watakapofanikisha kupatikana watuhumiwa au kutoa maelezo yanayofanikisha kumpata.

Imekuwa ni kawaida kwa vile kesi hizo hazina mwenyewe zinamalizika kinyemela mitaani.

## MAELEKEZO YA DC

Uchunguzi unaofanywa na Nipashe unabaini kuwa kesi hizo kwa maelekezo yaliyokuwapo zinashughulikiwa na wakuu wa shule pamoja na wa wilaya ni vyema kuongeza watendaji wengine ili kushirikiana na polisi kuwafikisha mahakamani.

Kwa hiyo inapotokea jitihada zimefanywa kumkamata na kumfikisha polisi na baadaye mahakamani, suala la nani mwenye jukumu la kumshitaki mtuhumiwa mbali na polisi linahitaji kuwekwa wazi licha ya Mkuu wa Shule kutakiwa atoe taarifa kwa Mkuu wa Wilaya, bado wanatakiwa wadau wengine ili kuwajibika zaidi.

Wakati mwingine kukosekana msimamizi wa kesi hizo kunaweza kusababisha wengi wasiziripoti polisi au wazazi na walezi kumalizana nje ya mahakama.

Licha ya polisi au Jamhuri kushughulikia kesi zinakwama kwa kukosa ushirikiano baina ya wazazi, walezi, wananchi, shule na hilo husababisha watu kutokomea.

Kwa vile si wazazi wala wananchi, shule au viongozi wa vijiji wanaohusika moja kwa moja vimbwanga vinaweza kutokea na kesi ikaishia hewani na wakati mwingine watuhumiwa kuruka dhamana na kutoweka.

Ni vyema kuja na mbinu mpya kuepusha kumaliza kesi hizo kabla ya kufikishwa mahakamani kudhibi baadhi ya wazazi na walezi wanaopokea rushwa, ng'ombe na mali nyingine ili kuwalinda watuhumiwa na wakati mwingine viongozi, walimu na polisi wakidaiwa kushiriki.

Jamii za wafugaji zinadaiwa kuwa mstari wa mbele kuficha ushahidi wa mimba za watoto wakitumia mbinu kama kuomba uhamisho kuficha mimba.

Ujanja huo unapelekea binti kuondoka shuleni bila taarifa za mimba kufahamika lakini baadaye kuonekana ana mtoto au ameolewa, na yote hayo huifichwa na walezi, wazazi na viongozi.

Wapo wanaowaficha mabinti wajawazito kwa kuwakataza wasiende shuleni ili wafukuzwe kwa sababu ya utoro sugu hayo nayo yamulikwe.

## ATHARI ZINAZOTOKEA

Japo zimeelezwa mara kwa mara kuna athari kisaikolojia na kimwili ikiwamo kupoteza maisha, huzuni na binti kujuta .

Aidha, wanakosa masomo, kuhangaika kutafuta riziki na chakula, mtoto kukosa malezi bora, binti kuingia kwenye biashara mitaani na mtoto mgongoni.

Mabinti kuwa wahalifu, kuambukizwa maradhi ya ngono na VVU.

## CHA KUIMARISHA

Ni wakati kwa serikali kuajiri maofisa maendeleo ya jamii shuleni iwe sekondari na msingi ili kusaidia wanafunzi masuala ya kijamii, ili kuyagundua matatizo na kuwaeleza wazazi na walimu ili yatatuliwe.

TEKNOLOJIA
NA DK FELICIAN KILAHAMA

# Ajabu Watanzania kuishi kinadharia kwa TEHAMA

PAMOJA na rasilimali na nguvukazi ya kutosha Watanzania wajiulize kwa miaka karibu 60 ya Uhuru na leo 57 ya Muungano wanatumiaje rasilimali hizo na nguvukazi mijini na vijijini kuondoa umaskini na kujiletea maendeleo?

Ni takribani miaka 60 tangu Uhuru uliopatikana Desemba 9, 1961, lakini maisha ya Watanzania na Wazanzibari ni ya kusuasua.

Wakati uhuru ulipopatikana masuala ya kiteknolojia hususani ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yalikuwa hayajashamiri kama ilivyo sasa.

Ukweli ni kwamba kutokana na hali hiyo Watanzania waliishi maisha halisi kama maandiko yanavyowataka - "kwa jasho mtu atapata riziki asiyetaka kufanya kazi asile".

Maagizo hayo yanamaanisha kama huna tatizo kiafya, lakini hutaki kufanya kazi ili kupata "mkate wa kila siku" lakini unalazimisha kupata chakula.

Hilo halikubaliki maana ni kulea uzembe, wizi, unyang'anyi na uporaji kwa kutumia nguvu. Kinachotakiwa ni kutimiza matakwa ya kanuni kwamba kila mwenye afya na nguvu afanye kazi ili kwa jasho lake amudu maisha na kukidhi mahitaji ya familia yake.



Vijana wanapata pesa kwa kutegemea simu na kompyuta wakiingiza muziki na kuonyesha picha za video. **PICHA: MTANDAO**

### MAENDELEO KITEKNOLOJIA

Nyakati hizi ni tofauti na zamani, mathalani, miaka 40 iliyopita na hasa katika kipindi cha miongo miwili iliyopita kumekuwapo na mageuzi makubwa na maendeleo ya teknolojia kiasi cha kusababisha baadhi kuishi kutegemea maendeleo hayo ambayo chanzo chake ni ugunduzi wa nchi zilizoendelea.

Nchi hizo ni mataifa yenye uchumi mkubwa maarufu G20 ambayo uchumi wao hutegemea uzalishaji bidhaa viwandani na matumizi makubwa ya TEHAMA na kusababisha kufanyika maboresho ya huduma za jamii kwa gharama nafuu.

### VIJANA WAATHIRIKA

Nchi zinazoinukia kiuchumi mfano Tanzania zimejikuta zipo katika hali ngumu kumudu maisha kwa sababu vijana maisha wanayoyajua ni "maliza kila kitu kiganjani" kwa mantiki kuwa kupata riziki ya kila siku kwa kutegemea teknolojia za kielekitroniki na TEHAMA kwa kutumia simu janja na kompyuta.

> Miaka 57 ya Muungano kuelekea 60 ya Uhuru Watanzania wajitathmini na kuweka bayana mwelekeo na mstakabali wa maendeleo yao.

Wengi wanazo ndoto kufanikisha maisha ya kila siku lakini ndoto hizo au maono haviendani na hali halisi kwa mazingira yalivyopo.

Kinachoonekana ni kujazana mijini kwa kuiga maisha kama yalivyo kwenye mataifa ya Ulaya na Marekani au Canada.

Watanzania wanajikuta katika hali hiyo ya maisha bila kuchunguza na kujiuliza walifikiaje?

Je,walifanyaje au walitumia mbinu gani hadi wakafikia hali ya maisha kama wanavyoona sasa?

Takribani miaka 200 iliyopita walikuwa katika mahangaiko kama wengi waliyo nayo sasa.

### MAENDELEO ENDELEVU

Kupata maendeleo endelevu, haikuwa kazi rahisi watu walihangaika mpaka wakafika Afrika kujipatia rasilimali pamoja na nguvukazi ambao ni watumwa ili wafanye kazi, leo ni raia wa Marekani na kwingineko duniani wanaotajwa kuwa wana asili ya Afrika.

Hivyo, Afrika ilichangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kiuchumi katika mabara ya Ulaya, Marekani na Uarabuni.

Kinachotokea sasa ni kama Watanzania wamejenga ndoto zao kwa namna ya kuyamudu maisha yao ya kila siku kana kwamba wako sawa na nchi zenye mapinduzi makubwa ya kiteknolojia na kutaka wafanane nao kwa kila hali wakati hata uwezekano wa kwenda kuchukua rasilimali au teknolojia kutoka kwao, ni finyu au haupo.

Ndoto za kuishi mijini kwa kutegemea yanayotokana na mafanikio katika nchi zenye nguvu za kisayansi na teknolojia ni kama kuota mchana.

Itakumbukwa waliokuwa wakistaafu utumishi miaka ya nyuma walikuwa wanaishi vijijini.

Leo wastaafu na wengine wanatamba, "tutabanana hapahapa," wachache wanarejea vijijini. Isitoshe vijana walioko vijijini wanatamani waje wakae mijini kisa? Urahisi wa kumudu maisha kwa dhana ya mambo kiganjani na simu janja.

### KINACHOFANYIKA

Pamoja na shughuli halali za kompyuta na simu kuna wengi wanaozitumia kuhadaa watu kuwa wameshinda shindano watume hela kupata taarifa, wengine hutuma ujumbe wa 'kurushiwa fedha kwa namba hii'. Kuna wanaotangaza taarifa waganga wa kienyeni wakati baadhi hutumia kompyuta kuingiza miziki, kuonyesha picha zisizo na maadili kwenye vibanda.

### FIKRA ZA KUJITEGEMEA

Wakati John Magufuli, alipoingia kwenye awamu ya kwanza ya urais, serikali aliyoiongoza utendaji kazi wake ulidhihirisha kuwa watu wakidhamiria wanaweza kujiletea maendeleo yao wenyewe bila kutegemea misaada au uwekezaji wenye masharti magumu na kandamizi.

Magufuli alikusudia huduma zote muhimu zipatikane vijijini na Watanzania kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo endelevu.

Kwenye kipindi cha kwanza alibainisha kuwa "penye nia pana njia" na Watanzania wanaendelea kuamini awamu ya sita itawafikisha kwenye uhalisia wa maisha.

Mathalani, serikali ilitarajia kuwa ifikapo 2025 umeme wa gharama nafuu uwe umevifikia vijiji vyote, hilo pia litatekelezwa.

Barabara za uhakika ziwe zimefika vijjini; huduma muhimu, maji, afya, elimu, benki, miundombinu ya biashara na masoko ya mazao ya kilimo na mifugo zikiwamo huduma za ugani na uperembaji, yote hayo yawe yapatikane kirahisi kwa wakulima na wafugaji.

Hayo yote yanatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassani, atasimamia na ilani ya CCM itatekelezwa ipasavyo na taifa kusonga mbele.

### KUANZIA LEO

Ni vyema kuishi kwa ndoto au maono ya Kitanzania maana ni vigumu kuishi kwa ndoto za 'ulimwengu' mwingine badala ya ukweli kulingana na uhalisia wa maono na hisia za Kitanzania.

Hata hivyo, maisha ya kisayansi na teknolojia hayakwepeki, ni mtazamo mzuri lakini watu wawe waangalifu wasiende bila mikakati. tena waondokane na ndoto zisizo sahihi kulingana na uhalisia wa mazingira yaliyopo.

Tahadhari ni muhimu kukwepa kuangamia kwa kukosa maarifa au kuwa na maono potofu.

Miaka 57 ya Muungano kuelekea 60 ya Uhuru Watanzania wajitathmini na kuweka bayana mwelekeo na mstakabali wa maendeleo yao.

Ni wakati wa kuwa na uwiano linganifu wa maendeleo mijini na vijijini (balanced development), ili walioko vijijini wasijisikie vibaya bali wafurahi na wanaposema utalii wa ndani uanzie hapo, mwananchi atoke kijijni aje kufurahia maisha kwenye jiji au mji anaoupenda na baadaye kurejea alikotoka.

Kadhalika, waliopo mijini wavinjari vijijini na kufurahia maisha na kudhihirisha kuwa Tanzania ni nchi yenye maziwa na asali. Wawekezaji wajitokeze kuwekeza vijijini kwa nia ya kuinua maisha ya wanavijijini na kwa faida ya wote.

Wakati huohuo serikali iendeleze juhudi zake kuimarisha miundombinu na huduma za kijamii ikiwamo TEHAMA vijijini.



# Waziri Kalemani atangaza uamuzi mgumu TANESCO

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameliagiza Shirika la Umeme (TANESCO) kuvunja Bodi ya Manunuzi kuanzia juzi kutokana na kulalamikiwa kuwa na ukilitimba katika masuala ya manunuzi.

Dk. Kalemani aliyasema hayo jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na Mameneja wa TANESCO, Kanda, Mikoa pamoja na wilaya katika kikao kazi kilichofungwa juzi.

Alisema Bodi hiyo ya manunuzi imekuwa ikipigiwa kelele kutokana na ukilitimba uliopo hasa katika suala la manunuzi kutokana na baadhi ya kanuni kukiukwa. “Lazima bodi hii ivunjwe kuanzia leo, hii na ichaguliwe nyingine na ianze kazi leo hii manake kumekuwa na ukiritimba mkubwa katika manunuzi... anaachwa mtu mwenye bei ndogo katika manunuzi na kuchukuliwa mtu mwenye bei juu,” alisema Dk. Kalemani. Alisema pia pamoja na kuvunjwa kwa bodi hiyo anaagiza uchunguzi ufanyike kwa watu wote walikuwa wakilalamikiwa juu ya ukiukwaji wa sheria za manunuzi katika Bodi hiyo.

Aidha, aliwataka mameneja wote wa TANESCO kuhakikisha wanaongeza kasi ya usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini.

“Azma ya serikali ni huduma hii ya umeme ifikie vijiji vyote ifikapo Desemba 2022, hivyo kuanzia sasa tuna miezi 18, kukamilisha zoezi hili ili kuvifikia vijiji vyote vilivyo baki,” alisema.

Kadhalika, aliwataka mameneja wote ambao wanaona kuwa watashindwa kutimiza wajibu wao wa kupeleka umeme kwa wananchi wajitoe mapema kabla hawajaondolewa katika nafasi zao. Pia, alipiga marufu mgawo wa umeme na ukataji wa umeme bila kutoa taarifa kwa wananchi na atakayeshindwa kutimiza hilo ataipoteza nasafi yake. “Pamoja na suala la mgawo wa umeme na kukatika kwa umeme, lakini pia meneja ambaye atashindwa kuwaunganishia umeme wananchi ambao wamelipia kwa wakati, hatua kali zitachukuliwa ikiwamo kuondolewa katika nafasi yake,” alisema.

Katika hatua nyingine, Dk. Kalemani aliuagiza uongozi wa TANESCO kuhakikisha kuwa unaongeza jitihada katika ukusanyaji wa mapato.

Alisema hivi sasa ukusanyaji wa mapato katika shirika hilo umeongeza ukilinganisha na kipindi cha miaka mitano iliyopita, lakini bado ipo haja kuongeza jitihada.

“Ukusanyaji mapato miaka ya nyuma ulikua bilioni 9, kwa wiki, mwaka juzi ukawa Sh. bilioni 36 kwa wiki mwaka jana bilioni 39 kwa wiki lakini hivi sasa ni takribani Sh. bilioni 46 kwa wiki hivyo mnatakiwa kuongeza juhudi ikibidi tuwazidi hata TRA,” alisema Dk. Kalemani.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA), Mhandisi Advera Mwijage, alisema watahakikisha maagizo yote yaliyotolewa na Waziri wanayafanyia kazi ili wananchi wote wanufaike na nishati hiyo ya umeme.




Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Palamagamba Kabudi (kulia) akitoa mada kwenye Kongamano la miaka 57 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lililofanyika jana ukumbi wa mikutano Chimwaga Jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mavunde apiga jeki ujenzi wa shule

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, amekabidhi saruji tani 29, kwa Ofisa Elimu Msingi na Ofisa Elimu Sekondari, kusaidia ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo kwa shule za msingi na sekondari za Jiji la Dodoma.

Mbunge Mavunde amekabidhi saruji hizo zenye thamani ya Sh.milioni 10 na kuwataka walimu wakuu na viongozi wa kata husika kusimamia matumizi yake ili kufikia lengo lililokusudiwa.

“Mchango wangu huu ni kwa lengo la kuboresha sekta ya elimu na hasa katika ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo sambamba na kuunga mkono jitihada za wananchi za ujenzi wa shule mpya za msingi na sekondari, hivyo lazima ninyi viongozi msimamie matumizi sahihi ya vifaa hivi.

“Nitaendelea kuchangia kwenye sekta hii ya elimu ili kuwafanya wanafunzi wa Dodoma Jiji wasome katika mazingira ambayo ni rafiki, lakini pia tunaishukuru serikali kupitia TEA kwa kutupatia Sh. bilioni 1.9 za ujenzi wa madarasa na majengo ya utawala kwa shule 5 za msingi,” alisema Mavunde.

Wakishukuru kwa niaba ya wananchi, Madiwani Assedi Ndajilo wa Hombolo Bwawani na Charles Ngh’ambi wa Kata ya Mbalawala wamemshukuru Mbunge Mavunde kwa namna anavyochangia maendeleo ya sekta ya elimu katika kuweka mazingira mazuri ya wanafunzi kusoma.

Aidha waliahidi kusimamia vyema matumizi ya vifaa hivyo kwa malengo yaliyokusudiwa.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Ofisa Elimu Msingi, Joseph Mabeyo, amemshukuru Mbunge Mavunde kwa mchango wake mkubwa kwenye sekta ya elimu na kwa namna ambavyo amekuwa akishirikiana na idara za elimu msingi na sekondari kutatua changamoto mbalimbali.

# Wanafunzi wa zamani waisaidia shule yao meza

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADHI ya waliokuwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bihawana jijini Dodoma, wametoa msaada wa meza zaidi ya 30 kwa shule hiyo zikiwa ni jitihada za kuunga mkono serikali katika sekta ya elimu.

Akizungumza katika mahafali ya 17 ya kidato cha sita shuleni hapo Naibu Mkuu wa Chuo cha Serikali za Mitaa Taaluma, Utafiti na Ushauri, Dk. Michael Msendekwa, alisema maamuzi hayo yalifikiwa baada ya kutembelea shule hiyo na kuona inakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Dk. Msendekwa alisema meza hizo walizotoa 12, ni kwa ajili ya maabara na 20 ni kwa ajili bwalo la chakula.

Alisema wakiwa ni wadau wa elimu wanatambua kuwa hakuna Serikali inayoweza kufanya kila kitu kwa jamii bali kwa kushirikiana na wadau wengine.

“Mwaka jana tulifanya ziara ya kutembelea shule tuliyosoma tukaona kero mbalimbali moja wapo ilikuwa ni upungufu wa meza katika maabara na bwalo la chakula halikuwa na meza.

“Hii ilitufanya kuanza kuchangishana ili kutatua changamoto hizi, meza zote zimegharimu zaidi ya Sh.3 milioni,” alisema Dk. Msendekwa.

Aidha, aliwakumbusha wafanyakazi, wafanyabiashara pamoja na wengine kukumbuka shule walizosoma kwani nyingi zinakabiliwa na kero mbalimbali lengo ni kuisaidia serikali.

Naye Mhadhiri Chuo Kikuu cha St. John, Fredrick Golden, aliwaomba walimu pamoja na wanafunzi kulinda miundombinu katika shule hiyo kwa ajili ya wanafunzi wengine.

Aliishukuru serikali kwa ajili ya kuona umuhimu wa kuzifanyia ukarabati shule zote kongwe ikiwamo Bihawana kwa ajili ya kunufaisha watoto wao na vizazi vijavyo.

Aliiomba serikali kuziangali pia shule nyingine ikiwamo za kata ambazo zinakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo upungufu wa walimu, viti na meza na pale ambapo bajeti inaruhusu ifanye hivyo ili kuinua taaluma katika ubora unaotakiwa.

Mkuu wa shule hiyo, Joseph Mbilinyi, alisema shule hiyo ya wavulana kidato cha tano na sita ina wanafunzi 724 kati yao wahitimu ni 383.

Alisema licha ya shule hiyo kuwa na wanafunzi wengi walikuwa wanakabiliwa uhaba wa meza kwenye mbwalo kwani walikuwa wakitumia uwanja wa mpira kwa ajili ya chakula.

Aidha, alishukuru wanufaika hao kutatua kero hiyo ambapo pia alieleza baadhi ya kero zinazowakabili ikiwamo usafiri na upungufu wa walimu 15, wa masomo ya sayansi.





## 'Wapeni ushirikiano wasoma mita za maji'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BARAZA LA Ushauri wa watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA CCC) Mkoa wa Mbeya, limewataka wananchi mkoani hapa, kutoa ushirikiano kwa maofisa wa mamlaka ya maji wanaosoma mita za maji ili wapatiwe huduma wanayostahili.

Akizungumza na wandishi wa habari kwa niaba ya Mwenyekiti wa baraza hilo Mkoa wa Mbeya, Lusekelo Mwakyusa ambaye ni miongoni mwa wajumbe wa Baraza hilo, alisema baraza hilo lipo kwa ajili ya kuwatetea watumiaji wa huduma hizo pamoja na kuwashauri watoa huduma.

Alisema ili wawatetee vizuri wananchi ni lazima wananchi hao pia wawe na utaratibu wa kutoa ushirikiano ili kuepuka matatizo ikiwamo kubambikiziwa madeni na taasisi husika.

"Mwananchi akiwa na malalamiko juu ya huduma za nishati na maji anatakiwa kutuletea sisi akiwa na vielelezo ambavyo vitatusaidia sisi kuwa na pa kuanzia, tukishakuwa na vielelezo inakuwa rahisi kwetu kufuatilia," alisema Mwakyusa.

Alisema Baraza hilo lilianzishwa kwa mujibu wa sheria na kwamba lengo lake ni kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji pamoja na kuwashauri watumiaji hao.

Kwa upande wake Elizabeth Nyivambe, mmoja wa wajumbe walioongozana na Mwakyusa, alisema wamekuwa wakipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wakiwalalamikia watoa huduma hasa mamlaka ya maji.

Alisema wananchi wamekuwa wakilalamikia maofisa wa mamlaka hiyo kukadiria gharama za maji badala ya kwenda kusoma dira za maji kwenye makazi ya wananchi.

Alisema ili wananchi waepuke ongezeko la gharama za maji, wanatakiwa wafuate taratibu za kuepuka ikiwamo kuhakikisha wanafunga mabomba yao ili maji yasivuje.

# Sababu za kukosekana takwimu sahihi za vifo hizi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa Watanzania wengi hawana utaratibu wa kusajili vifo vya ndugu zao, hali ambayo inasababisha Serikali kukosa kumbukumbu na takwimu sahihi za vifo.

Kadhalika hali hiyo inachangia wanafamilia kukosa baadhi ya haki zao.

Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA), Emmy Hudson, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi mbalimbali wa Serikali kutoka katika wilaya zote za Mkoa huo kuhusu usajili wa vizazi na vifo kwa kutumia mfumo wa Tehama.

Alisema kwa mujibu wa Sheria yua Usajili wa vizazi na Vifo, ni lazima kila kifo kisajiliwe ili takwimu sahihi ziingizwe kwenye daftari la msajili mkuu wa Serikali ikiwamo sababu ya kifo cha mtu husika, umri wake pamoja na eneo kilipotokea.

Alisema kila kifo kinapotokea huwa kinatolewa cheti cha kifo ambacho ndicho kinathibitisha kwamba mtu husika amefariki, na kwamba cheti hicho huwa ni muhimu kwa wanafamilia kwa maelezo kuwa kinawasaidia kupata baadhi ya haki zao muhimu.

Emmy alisema Watanzania wengi huwa wanapuuzia cheti hicho kwa kujua ama kutokujua, huku baadhi wakiwa hawajui kabisa umuhimu wa cheti hicho.

"Faida ya nyaraka hiyo (cheti cha kifo) ni pamoja na kuwasaidia wanafamilia kufuatilia taratibu za mirathi, wanafamilia kulipwa mafao na pensheni pamoja na kupata malipo ya bima kwa marehemu ambaye bahati mbaya alifariki kwa ajali," alisema Emmy.

Vilevile, alisema nyaraka hiyo inawasaidia pia watoto ambao wanajiunga na elimu ya juu kunufaika na mikopo kutokana na mikopo hiyo kuwanufaisha zaidi watoto wa masikini.

Mratibu wa Vizazi na vifo kutoka katika Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Bhaskar Mishra, alisema usajili wa vizazi na vifo ni matukio ambayo yanatakiwa kwenda pamoja ili Taifa liwe na taarifa sahihi na kuwa na mipango sahihi.

Alisema Shirika hilo limekuwa likishirikiana na Serikali kuboresha mifumo ya usajili wa vizazi tangu mwaka 2013 kama sehemu ya majaribio katika Mkoa wa Mbeya na kwamba Shirika hilo litaendelea kushirikiana na serikali kwenye zoezi hilo.

Alisema wamekuwa wakifuatilia mfumo huo wa usajili ili kujua ufanisi wake na wamebaini kuwa una mafanikio mazuri, hivyo aliwataka watendaji kuendelea kuutumia.

"Kabla ya kuja Mbeya tulianzia kutoa mafunzo haya katika mikoa ya Iringa na Njombe ambako mfumo umefanikiwa kwa asilimia 100 na sasa baada ya Mbeya tutaingia Mkoa wa Songwe," alisema Mishra.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, alisema mfumo wa usajili wa watoto katika Mkoa huo una mafanikio makubwa, na kwamba baadhi ya Halmashauri zimefikia asilimia zaidi ya 90.

Alisema usajili wa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano ni bure na ni haki ya kila mtoto kusajiliwa na kupatiwa cheti chake ili kimsaidie kwenye maisha yake.



Askofu Mkuu Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya, Gervas Nyaisonga, akikata utepe juzi katika Kanisa Katoliki Parokia ya Roho Mtakatifu ya jijini Mbeya, kuashiria kuzinduliwa rasmi kwa mashindano ya mbio maarufu kama Marathon yaliyoandaliwa na Kanisa hilo kwa ajili ya kukusanya fedha za kuendeshea Redio Maria inayomilikiwa na Kanisa hilo. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# Makongolosi wakombolewa huduma za afya

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKAZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, wamepunguziwa adha ya kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 39 kwenda kupata huduma za afya kwenye Hospitali ya Wilaya hiyo baada ya kampuni ya ujenzi kuwajengea Kituo cha Afya chenye thamani ya Sh. milioni 250.

Kituo hicho kimejengwa na Kampuni ya China Railway 15 Bureau Group Corporation, inayojenga barabara ya Chunya-Makongolosi kwa kiwango cha lami, huku Halmashauri ya wilaya hiyo pia ikichangia ujenzi wa baadhi ya majengo.

Akiwa katika ziara ya kukagua ujenzi wa barabara hiyo mwishoni mwa wiki, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Leonard Chamriho, alitembelea kituo hicho cha afya kwa ajili ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua mradi huo, alisema kampuni hiyo ilijenga kituo hicho kama sehemu ya utekelezaji wa agizo la aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli kwa kampuni hiyo.

Alisema kampuni hiyo ilikubali kujenga kituo hicho kama sehemu ya kurudisha faida kwenye jamii ambayo wanashirikiana nayo kwenye ujenzi wa barabara hiyo.

"Kwa sababu hii ilikuwa ni ahadi ya aliyekuwa rais wetu Hayati Dk. Magufuli, pia tutamuomba Rais wetu, Samia Suluhu Hassan aje atufungulie kituo hiki bora kabisa," alisema Mhandisi Chamriho.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Saimon, alisema mchango wa kampuni hiyo wa kujenga Kituo cha Afya umeacha alama kubwa kwa wakazi wa Mji huo Mdogo wa Makongolosi ambao kwa muda mrefu ulikuwa hauna kituo kikubwa kama hicho.

Alisema kituo hicho kitasaidia kuhudumia wananchi wa Mji huo wa Makongolosi pamoja na maeneo jirani zikiwamo Kata za pembezoni ambazo bado hazina vituo vya afya.

Alisema Mji wa Makongolosi kwa sasa una ongezeko kubwa la watu kutokana na shughuli za kijamii, hivyo kulikuwa na uhitaji mkubwa wa kituo cha afya chenye hadhi inayoendana na idadi ya watu waliopo.

"Kuna kata nne za Mji huu ambazo zote hazina vituo vya afya na hivyo wananchi wote wa maeneo haya walikuwa wanahudumiwa na Zahanati ya Makongolosi, sasa kampuni hii imewapunguzia wananchi hawa tatizo," alisema Mayeka.

Alisema mbali na kituo hicho pia kipo kituo cha afya ambacho kinajengwa na serikali, na kwamba vituo hivyo kwa pamoja vitasaidia kuokoa maisha ya wananchi hasa wanawake na watoto ambao alidai ndio huwa wanapata shida zaidi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Sophia Kumbuli, alisema kituo hicho kitakuwa kinahudumia zaidi ya wananchi 12,000 wa Mji wa Makongolosi.

Kumbuli aliwashukuru wananchi wa Mji huo kwa ushirikiano wanaoendelea kuuonyesha kwa wakandarasi hao ambao wamewasaidia kituo hicho cha afya.

Mei 2019, Hayati Dk. Magufuli alifanya ziara wilayani Chunya na kuitaka Kampuni hiyo ya kichina kuwasaidia wananchi wa Mji wa Makongolosi kama mchango wao kwa jamii.



# Othman asisitiza umoja Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema Zanzibar inahitaji kuendelea na umoja ili maendeleo yapatikane kwa haraka.

Aliyasema hayo jana baada ya kukamilisha ziara ilioandaliwa na Chama cha ACT-Wazalendo kwa ajili ya kuwatembelea wagonjwa katika maeneo mbalimbali ya Unguja.

Alisema hakuna njia nyingine itakayoweza kuleta maendeleo bila kuwapo ushirikiano, upendo na umoja miongoni mwa Wazanzibari.

Alieleza kuwa yupo tayari kutoa mchango wake kwa kuwatumikia wananchi na anamini wananchi nao wapo tayari kuendeleza upendo na amani ya nchi yao.

"Na mimi naweka ahadi ya kuwatumikia Wazanzibari kwa wakati wowote ili kuendeleza yale yaliyoanzishwa na kuleta tija katika muendelezo wa kuyaimarisha zaidi," alisema Othaman.

Alieleza kuwa anaweza kutoa mchango wake katika kutumikia watu na kufanyakazi ya kuwatumikia wananchi ili malengo ya uweao umoja wa kitaifa kufikiwa.

"Umoja na upendo ndio silaha pekee ya uwapo wa amani ya kudumu katika taifa lolote lile duniani," alisema.

Alisema upendo na umoja huo unapendeza zaidi watu wakitembeleana na kusaidiana kwa wale wanaohitaji msaada.

Alisema mgonjwa yeyote akiona anatembelewa na jamaa zake au majirani, marafiki hujisikia faraja kupunguza maumivu ya maradhi.

Aliwashauri wananchi wa Zanzibar katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani ni vyema kifuturu pamoja ili kuwa karibu zaidi na kuwasitiri wale wasio na uwezo.

Alisema kuna watu wengi hawana chakula cha futari, lakini iwapo utamaduni wa kufuturu pamoja utaendelea, utaleta faida kubwa miongoni mwao.

Katika ziara hiyo ya kuangalia na kuwafariji wagonjwa katika vijiji vya Mkoa wa Kaskazini Unguja, Makamu wa Kwanza aliwatembelea wagonjwa katika vijiji vya Chaani, Matemwe, Nungwi, Kendwa, Kilimani Tazari, Mahonda, Bumbwini Mafufuni na Kiomba Mvua.



Rama Jumanne Muna (kushoto) akichangia kwenye mkutano wa kwanza wa utambuzi na uandikishaji wa Kaya masikini kwenye ukumbi wa Ngome kongwe Mjini Zanzibar Jana. Kulia Ni Salma Abdalla Haji, Mwezeshaji wa Tasaf. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Z'bar yashiriki kampeni chanjo ya watoto Afrika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR imeungana na mataifa mengine ya Afrika katika uzinduzi wa wiki ya kampeni ya chanjo Afrika iliyoanza jana.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema lengo la kampeni hiyo ni kuongeza msisitizo wa kuwapatia chanjo watoto wote ili kuwakinga na maradhi mbalimbali yanayoweza kuzuilika kwa chanjo.

Aliwataja wahusika wa kampeni ya chanjo Afrika kuwa ni watoto waliofikia umri wa miaka miwili, miaka mitano ambao hawajakamilisha na kwa wasichana wenye umri wa miaka 14.

Waziri Mazrui alisema chanjo ni mkakati mwafaka wa kupunguza maradhi mbalimbali yanayozuilika kwa njia hiyo na kupunguza vifo vya watoto.

Alisema Zanzibar imefanikiwa kwa asilimia 90 kuwapatia chanjo watoto wanaostahiki hata hivyo bado wapo watoto ambao hawajapata kabisa chanjo yoyote, hivyo aliwataka wazazi na walezi kuitumia fursa ya wiki ya chanjo Afrika kuwapeleka vijana wao kwenye vituo vya kupatiwa chanjo.

Aliizitaja Wilaya za Mjini, Micheweni, Magharibi 'A' na Magharibi 'B' kuwa hazikufikia lengo lililopangwa na Serikali la kuwapatia chanjo watoto mwaka uliopita 2020.

Aliwataka viongozi na watendaji wote kuchukua juhudi ya kusimamia kampeni hiyo kwa sababu kujikinga na maradhi ni kuipunguzia serikali na familia gharama kubwa za matibabu zisizo za lazima.

Naye Ofisa wa Chanjo wa Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), Emannuel Tessua, alisema mpango wa Taifa wa chanjo ulianza mwaka 1985 kwa chanjo tano kwa ajili ya kuwakinga watoto na maradhi matano na hadi kufikia mwaka jana kuna chanjo tisa zenye uwezo wa kukinga maradhi 13.

Aliyataja maradhi yanayokingwa na chanjo hizo kuwa ni polio, surua, rubela, pepopunda, dondakoo, kifua kikuu, kuharisha, kichomi, saratani ya mlango wa kizazi , homa ya ini na mafua makali.

Kaulimbiu ya Wiki ya Chanjo Afrika kwa mwaka 2021 ni 'Chanjo huiweka jamii pamoja'.

# Waliodhalilishwa watakiwa kusoma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA elimu mjumuisho kwa watu wenye ulemavu Kisiwani Pemba, Ali Khamis Kombo, amewataka watoto waliofanyiwa vitendo vya udhalilishaji kuendelea na masomo yao.

Amesema kupatwa na kadhia hiyo isiwe sababu ya kutojiendeleza kielimu.

Aliyasema hayo katika Ofisi ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Ofisi ya Pemba, baada ya kukutana na watoto ambao wamepatwa na kadhia hiyo.

Alieleza vitendo vya udhalilishaji vimekuwa kama wimbo wa Taifa kila siku vinajitokeza ndani ya jamii, hasa kwa watoto kuanzia miaka mitano hadi 18, jambo ambalo linawapa wakati mgumu Serikali na jamii.

Alisema kwa wale ambao Mungu amewapa mtihani huo si jambo la busara kukata tamaa ya maisha na kukataa kwenda shule na badala yake kurejea shule kuendelea na masomo yao ili wafikie ndoto zao.

Aidha alisema kwa wale ambao hawendi tena shule kutokana na kufikwa na kadhia hiyo waendelee kusoma, ili kutimiza ndoto zao za maisha yaliyo bora kwa maendeleo yao.

"Kitendo cha kudhalilishwa ni kitendo kibaya na kisichosahaulika maishani, lakini isiwe chanzo na sababu ya kukata tamaa kabisa ya kutofikia malengo na ndoto zanu kimaisha," alieleza.

Aliwanasihi waathirika hao kuwa kila wanapoendelea kuishi na kuwa karibu na jamii, wasijiachie na kujisahau kabisa na kuamini kila mtu kuwa ni mwema katika maisha yao na kutokubali kuendelea kufanyiwa tena vitendo hivyo.

Naye Ofisa Ushauri Nasaha kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake Pemba, Khamis Ali Omar, alisema kitendo cha udhalilishaji bado ni kadhia kubwa kwa watoto, Serikali na jamii kwa ujumla, kitendo ambacho hakisahauliki katika maisha yote ya duniani.

"Watoto wengi sasa hivi ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar wamekuwa wakiathirika zaidi kisaikolojia na kupoteza ufahamu na mwelekeo wa malengo waliyokwisha kujipangia kimaisha,"alisema.

Mshauri huyo aliwataka watoto hao, kwamba lengo lao ni kuwasaidia, hivyo wasione aibu kutoa taarifa mapema kwenye vyombo husika, ama kwa wazazi wao pale anapotokea mtu kutaka kujaribu kuwafanyia vitendo hivyo, ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Mratibu wa TAMWA Ofisi ya Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema kuwa bado vitendo hivyo ni changamoto kwa watoto, jambo ambalo linawapa wakati mgumu watoto hao kufikia ndoto zao.

Alisema ipo haja kwa wazazi na walezi pamoja na taasisi nyingine binafsi na za serikali, kutoa ushirikiano katika kupambana na tatizo hilo na kutoa ushirikiano, pale wanapohitajika kwenye vyombo vya sheria ikiwamo mahakamani kutoa ushahidi ili haki itendeke.

Watoto hao waliodhalilishwa, walisema kuwa kesi zao bado zinakabiliwa na changamoto zinazosababishwa na baadhi ya watendaji wa serikali na baadhi ya kesi hizo kufutwa bila haki kutendeka.

Hata hivyo,waliiomba Serikali ya kuendelea kuwa na msimamo wa kusimamia sheria za kesi hizo,na kuwachukulia hatua wenye tabia ya kuingilia kati kesi za udhalilishaji wakiwa na lengo la kupotosha ushahidi, ili iwe funzo kwao na kwa wengine wenye tabia kama hiyo.

Aidha,walisema wanaona aibu kwenda shule kuendelea na masomo kwa sababu baadhi ya watoto wezao huwaonyeshea vidole, jambo ambalo huwafanya kuwa wanyonge na kutokuwa na furaha.

# ALAT yataka madiwani kuzungumzia maslahi

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

KATIBU wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Elirehema Kaaya, amewataka madiwani kuibua suala la maslahi kwenye vikao vya ALAT mkoa ili liweze kushughulikia kwa haraka

Kaaya aliyasema hayo jana katika Halmashauri ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo, wakati wa ziara ya siku moja kukagua miradi ya maendeleo ya kimkakati ambayo utekelezaji wake unaendelea.

Alisema katika ziara zake alizofanya kwenye halmashauri, ajenda ya maslahi imekuwa ikizungumziwa na madiwani jambo ambalo limeonekana kuwa linatakiwa kufanyia maboresho.

Kaaya alisema kikao vya ALAT mkoa ajenda hiyo ikipewa kipaumbele ikafikia ngazi yake ataichukua na kumfikishia Waziri ambaye atafikisha kwa Rais kuomba maboresho ya maslahi yao.

"Nimepata malalamiko kutoka kwa Wenyeviti wa Halmashauri kuhusiana na maslahi nimewashauri kupitia kwa viongozi wao wa ALAT wawasilishe malalamiko yao ili lifanyiwe kazi, jambo hili limepokelewa na litafanyiwa kazi, wavute subira serikali imeshalipokea," alisisitiza.

Aidha, alisema ameridhika na miradi aliyotembelea ambayo ni mradi wa soko la kisasa, kituo kikuu cha mabasi na Hospitali ya Wilaya ya Msoga.

Akiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Msoga alishauri kufanyika ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua ili isaidie kwa matumizi ya Hospitali hiyo pamoja na kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

Naye, Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, alimuomba Katibu huyo kuwafanyia marekebisho kwenye makusanyo ili mapato halali yabaki katika Halmashauri hiyo yatekeleze miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Geoffrey Kamugisha, alimpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kwa kutekeleza mapendekezo ya Madiwani ambayo yamesababisha kuwapo kwa utekelezaji wa miradi mikubwa katika Halmashauri hiyo.

Alisema malengo yao kwa miaka mitano ijayo ni kukusanya Sh. Bilioni 20, kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato.

Naye, Diwani wa Miono, Juma Mpwimbwi, pamoja na madiwani waliohudhuria katika ziara hiyo waliomba serikali kuwaboreshea maslahi.








Wananchi wa Kijiji cha Mpeta wakiagana kwa furaha na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (katikati kulia), muda mfupi baada ya kumalizika kwa mkutano wa Waziri huyo na Wananchi wa Kijiji hicho uliofanyika wilayani Uvinza, Mkoani Kigoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto anayedaiwa kubakwa na babu aomba msaada

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MTOTO wa kike mwenye umri wa miaka mitano mkazi wa Kijiji Katuruka, Bukoba Vijijini (jina linahifadhiwa), amepatwa na tatizo la kutokwa na mkojo muda wote baada ya madai ya kubakwa na mtu anayetajwa kuwa ni ndugu wa karibu wa mama mzazi wa mtoto huyo.

Akizungumzia tatizo hilo, bibi wa mtoto huyo, Joines Habibu, alisema siku ya tukio Februari 19, mwaka huu, aliondoka kwenda kanisani na kumuacha mjukuu wake nyumbani kwa mtuhumiwa, na kwamba aliporudi wakati akimwogesha mtoto huyo saa nne usiku alianza kupiga kelele akidai anaumia.

Bibi huyo alisema kuwa baada ya mjukuu wake kumwambia kuwa ana maumivu katika sehemu zake za siri, aliamua kumkagua ili kujua ana tatizo gani na alipofuatilia aliona hali isiyo ya kawaida katika sehemu zake za siri.

"Mjukuu wangu aliendelea kulia na kuomba apelekwe hospitali, nikamuuliza hayo maumivu yametokana na nini akanieleza kwamba babu yake ambaye ni baba mdogo wa mama yake mzazi, alimlaza na kumwingizia kimti kigumu katika sehemu zake za siri," alisema.

Alisema baada ya kupewa taarifa hiyo, alikwenda kwa Mwenyekiti wa kijiji hicho na kupewa barua ya kwenda polisi kutoa taarifa, lakini hadi sasa mtuhumiwa hajakamatwa.

"Kinachoniuma zaidi mjukuu wangu baada ya kubakwa alipatwa na tatizo muda wote mkojo unatoka, tunalazimika kukaa tumemfunga madaso (nepi) ili asichafue nguo, lakini bado anatoa harufu hata tukimsafisha," alisema bibi huyo.

Alisema baada ya kubakwa alipelekwa hospitali akatibiwa na pia kupewa dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi (ARV) ambazo alizimeza kwa muda wa siku 30 kwa lengo la kuzuia maambukizi ya ugonjwa huo.

Alisema, baada ya kuona tatizo la kutokwa na mkojo linaendelea alimrudisha hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Kagera na kuambiwa kuwa inabidi mtoto huyo apewe rufaa kwenda hospitali ya kanda Bugando, mkoani Mwanza.

"Niliwaambia sina uwezo wa kumpeleka huko, wakanijibu niondoke nijiandae nikipata uwezo nirudi hospitali ili aandikiwe rufaa, lakini hadi sasa sijarudi kwa sababu sina uwezo wa kifedha wa kwenda Bugando, naomba Watanzania wanisaidie," alisema.

Mama mzazi wa mtoto huyo, Angela Habibu, alisema kuwa miaka yote huwa anaishi na mtoto wake, lakini alimpeleka kwa bibi yake kwa muda na alikuwa hajamfuata, hadi alipopewa taarifa kuwa mtoto wake amebakwa.

Aliomba mtu yeyote anayeweza kumsaidia amtafute kwa namba ***0769397935*** au ***0743873448***.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Maketi Msangi, alithibitisha kulifahamu tukio hilo na kudai kuwa hadi sasa wanaendelea kumsaka mtuhumiwa huyo, Mushobozi Mpambanza, anayetajwa kuwa ni baba mdogo wa mama mzazi wa mtoto huyo, ambaye alitoroka baada ya tukio.

"Tukio hili liliripotiwa katika kituo cha polisi Bukoba Februari 20, mwaka huu, tunalo na tunaendelea kulifanyia kazi, mtuhumiwa akikamatwa hatua za kisheria zitaendelea ikiwamo kumfikisha mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili" alisema Msangi.

Mganga mfawidhi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera, Dk. Mseleta Nyakiroto, alisema walimpokea mtoto huyo Februari 20, mwaka huu na kumpatia matibabu ya tatizo alilokuwa nalo ambalo hakulitaja na kisha kumruhusu.

"Mtoto huyo hajaandikiwa rufaa kwa sababu tulimtibu tatizo alikokuja nalo na tukamruhusu, kama sasa ana tatizo jingine basi aletwe tena hospitali akatibiwe au ikionekana hawezi kutibiwa hapa tumpe rufaa ya kwenda hospitali kubwa zaidi," alisema Nyakiroto.

HABARI KIMATAIFA

# Matumizi ya kijeshi yaongezeka duniani

PAMOJA na uwapo wa janga la virusi vya corona, jumla ya matumizi ya zana za kijeshi duniani kwa mwaka uliopita, yameongezeka kwa karibu dola trilioni mbili.

Takwimu mpya zilizotolewa na Taasisi ya Kimataifa inayohusika na Utafiti wa Masuala ya Amani (SIPRI) yenye maskani yake mjini Stockholm, nchini Sweden.

Taarifa hiyo inasema kumekuwepo na jumla ya matumizi ya kiasi cha dola bilioni 1,981, na kufanya ongezeko la asilimia 2.6 ikilinganishwa na mwaka 2019. Mataifa ambayo yanaongoza katika matumzi makubwa ni Marekani, China, India, Urusi na Uingereza.

Yote kwa pamoja yanafanya jumla ya asilimia 62 ya jumla ya matumizi ya silaha duniani na kwa namna ya kipekee kiwango hicho kwa China kimekuwa kikiongezeka kwa takribani mwaka wa 26 kwa mfululizo.

Mtafiti wa SIPRI, anaehusika na Silaha na Programu ya Matumizi ya Kijeshi, Diego Lopes da Silva alisema janga la virusi la corona, halikuwa na athari zozote katika matumizi ya zana za kijeshi kwa mwaka 2020.

Hata hivyo aliongeza kuwa kwa sasa bado wapo katika tathmini ya endapo mataifa yataendelea katika kiwango hicho cha matumizi ya kijeshi katika kipindi hiki kingine chote cha corona.

Lakini pamoja na ongezeko hilo la fedha katika sekta ya ulinzi kwa mataifa mbalimbali lakini baadhi ya mataifa kwa kiwango kikubwa pia yalibadilisha fedha za bajeti zake kwa mpango huo na kuzielekeza katika jitihada za kukabiliana na janga la virusi vya corona.

Mfano wa mataifa yalichukua mkondo huo ni pamoja na Chile, Korea Kusini, mengine Brazil na Urusi. SIPR Iinasema mataifa hayo yalitumia kiwango cha chini kuliko kilichoainishwa awali kwa bajeti ya 2020.

Marekani ambayo inatajwa kuwa kinara wa kutumia fedha nyingi katika sekta yake ya ulinzi, kwa mujibu wa SIPRI kwa mwaka 2020, matumizi yake ya kijeshi yanakadiriwa kufikia dola bilioni 778 likiwa ni ongezeko la asilimia 4.4 ikilinganishwa na mwaka 2019.

Kwa hatua hiyo Marekani inahesabiwa kutumia asilimia 39, ya jumla ya asilima zote za matumizi ya kijeshi duniani. Hili pia ni ongezeko la mara ya tatu mfululizo, baada ya miaka mengine saba ya jitihada za kupunguza matumizi hayo. **DW**

**Mataifa ambayo yanaongoza katika matumzi makubwa ni Marekani, China, India, Urusi na Uingereza.**

# Kenya yasitisha kufunga kambi Dadaab, Kakuma

**Nairobi,** KENYA

SERIKALI ya Kenya imesema haitafunga kambi za wakimbizi za Dadaab na Kakuma, na kwamba inataka suluhisho.

Kamishna Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR), Filippo Grandi, alisema hayo alipotembelea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Rwanda na Burundi, ili kufahamu shida zinazowakabili wakimbizi katika maeneo hayo.

Mwezi uliopita, Kenya ilitoa siku 14 ya kufungwa kambi za Dadaab na Kakuma, ikitoa sababu za hofu ya kiusalama kwa kitaifa na wizara ya mambo ya ndani ilikuwa ikisema, hakuna nafasi ya mazungumzo zaidi.

Nchini Rwanda wiki iliyopita, Grandi aliwaambia waandishi wa habari kwamba wamekuwa na mazungumzo mazuri sana na serikali ya Kenya.

"Serikali ya Kenya haifungi kambi hizo, serikali ya Kenya inataka kupata suluhisho, wanataka kujua ni ipi njia bora ya kusonga mbele," Grandi alisema.

UNHCR limewasilisha kwa Kenya mipango ya baadaye ya kambi hizo mbili.

"Nadhani serikali ya Kenya itaendelea kutoa makazi... lakini inaeleweka wanataka kuwa na mkakati wa siku zijazo na mazungumzo yanaendelea."

Mapema mwezi huu, mahakama kuu ya Kenya iliripotiwa kuzuia kwa muda kufungwa kwa kambi hizo mbili za wakimbizi ambazo zinahifadhi zaidi ya 400,000.

**BBC**



Mji Mkuu wa Somalia, Mogadishu, jana ulikuwa shwari baada ya mapigano kati ya wanaounga mkono upinzani na vikosi vya usalama vya serikali, kwa mujibu wa redio binafsi nchini humo. **PICHA: BBC**

# Vikosi Somalia vyapigana kupinga muhula Farmajo

**Mogadishu,** SOMALIA

MAPIGANO yamezuka katika mji mkuu Mogadishu kati ya makundi kinzani ya vikosi vya usalama.

Ripoti zilisema kwamba silaha kali zilitumika huku makombora yakirushwa karibu na kasri la rais.

Baadhi ya vikosi hivyo vinamuunga Rais Mohammed Abdaullahi Mohammed, huku vingine vikimpinga.

Wiki iliyopita, Mohammed anayejulikana kama Farmajo kwa utata alijiongezea muda wake ofisini. Muhula wake uliisha rasmi mwezi Februari, mwaka huu.

Hatua hiyo ilikosolewa na jamii ya kimataifa ikiwamo Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU).

Ripoti kutoka Mogadishu siku ya Jumapili, wiki iliyopita, zilisema kwamba ghasia zilisambaa hadi katika maeneo mengine ya mji ikiwamo maeneo ya kati.

Vyombo vya habari nchini humo vilisema kwamba mapigano yalikuwa kati ya vikosi vya serikali na vitengo vya usalama ambavyo vinaunga mkono upinzani.

Ingawa baadhi ya wababe wa kivita na viongozi wa koo mbalimbali wanahusishwa katika ghasia hizo. **BBC**

# Wafanyakazi waliopotea na nyambizi wafariki

**Bali,** INDONESIA

SERIKALI ya Indonesia imetangaza kuwa wafanyakazi 53 waliopotea na nyambizi wamefariki baharini.

Maofisa hao walisema wafanyakazi waliokuwa ndani ya nyambizi iliyopotea Aprili 21, walifariki.

Nyambizi ya jeshi la wanamaji iliyotoweka katika pwani ya mji wa Bali siku ya Jumatano, wiki iliyopita, imepatikana ikiwa imekatika vipande vitatu chini ya bahari.

Maofisa wa wanamaji walisema kwamba walipokea ishara katika eneo ilipokuwapo nyambizi hiyo zaidi ya kina cha mita 800.

Gari la uokoaji wa chini ya maji lililokodishwa kutoka Singapore, lilitumwa chini ya maji kuthibitisha picha ya mabaki ya nyambizi hiyo. **TRT/BBC**



# PIRLO: SINA FURAHA JUVENTUS

**TURIN,** Italia

ANDREA Pirlo haamini kama mabosi wake wana furaha na namna Juventus inavyocheza baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, dhidi ya Fiorentina uliochezwa juzi.

Dusan Vlahovic aliwapa bao la kuongoza Fiorentina iliyopo kwenye hatari ya kushuka daraja kipindi cha kwanza pale katika dimba Artemio Franchi kwa mkwaju wa penalti baada ya Adrien Rabiot kuunawa eneo la hatari.

Kocha huyo wa Bianconeri, Pirlo akaamua kufanya mabadiliko baada ya kipindi cha kwanza kwa kuwatoa Leonardo Bonucci na Paulo Dybala, huku nafasi zao zikichukuliwa na Alvaro Morata na Dejan Kulusevski, na kubadilisha mfumo.

Mabadiliko hayo yalikuwa chanya na Morata akasawazisha bao ikiwa ni sekunde 31 tu baada ya kuingia, ingawa walishindwa kuondoka na pointi zote tatu.

Kabla ya mchezo huo, Mkurugenzi wa Juve, Fabio Paratici alibainisha kuwa nafasi ya Pirlo itakuwa salama kama watamaliza kwenye nne bora.

Pirlo amesema anajifunza kwenye kazi hiyo na anajua kwamba, amekuwa mbali na matarajio ya wengi katika msimu wake wa kwanza kwenye nafasi ya ukocha wa kikosi hicho.

Aliiambia Sky Italia: "Matarajio ya awali (wakati nachukua nafasi hii) yalikuwa tofauti na nafikiri nimefanya kazi ilivyotakiwa.

# Chelsea yaongoza mbio kumnasa Varane

**LONDON,** England

CHELSEA inaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Real Madrid, Raphael Varane dhidi ya Manchester United na Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa Mundo Deportivo.

Varane amekuwa na wakati mzuri kule Real Madrid, akishinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini sasa, Varane anaonekana kama vile ametosheka kucheza kwa miamba hao wa Hispania na sasa yupo kwenye rada za Chelsea.

Kwa mujibu wa ripoti, Chelsea wanaongoza na wapo kwenye nafasi kubwa zaidi ya kumsajili nyota huyo mshindi wa Kombe la Dunia na Ufaransa mwaka 2018 nchini Urusi.

Varane amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoka Madrid, ambao wanaonekana wanataka kuingiza fedha kwa ajili ya kumsajili nyota wa PSG, Kylian Mbappe na fowadi wa Borussia Dortmund, Erling Haaland.

United pia imeripotiwa kuwa kwenye mbio za kuwania saini ya beki huyo, lakini sasa Chelsea ndio wanaoaminika kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi.






# *Solskjaer ahofii kelele za mashabiki*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesisitiza timu yake haitaathiriwa na maandamano ya mashabiki dhidi ya wamiliki wa klabu kutokana na kujiunga na ligi mpya ya Ulaya.

Mashetani Wekundu hao walitoka suluhu na Leeds United kweye mchezo wa Ligi Kuu England pale kwenye dimba la Elland Road, juzi Jumapili.

Kabla ya mchezo huo, mashabiki waliandamana nje ya dimba la Old Trafford kushinikiza kujiuzulu kwa uongozi baada ya wamiliki, familia ya Glazer kuiingiza klabu hiyo kwenye ligi mpya ya Ulaya iliyozua utata kabla ya kufutwa.

Mashabiki wa United licha ya ligi hiyo kufutwa, lakini bado hasira zao wanapaza kwa familia ya Glazer na wakati wa mchezo huo, ndege ndogo iliyobeba bango lililoandikwa - "Bilioni 2 zimeibwa - Glazers ondokeni" - ilipita kwenye anga la Uwanja wa Elland Road kabla ya kuanza kwa mchezo.

Wakati United ikijiandaa na mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya AS Roma Alhamisi hii, Solskjaer aliulizwa kama maandamano hayo yanaweza kuwaathiri wachezaji wake kwa kipindi cha msimu kilichobaki.

"Kwa uhakika nina furaha kubwa na vijana wangu. Wanajua nini wanachotakiwa kufanya, kwani msimu umekuwa mgumu na imara sana," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Bila shaka yoyote tunajua umuhimu wa michuano ya Ulaya, na wachezaji wamejiandaa vizuri, hivyo hakuna tatizo lolote na hakutakuwa na athari yoyote kutokana na maandamano ya mashabiki.

United baada ya sare hiyo sasa wamepitwa pointi 10 na vinara Manchester City na wamewazidi pointi 13, Liverpool waliopo nafasi ya sita.

# DYBALA AFUNGUKA TABIA YA RONALDO




**TURIN,** Italia

PAULO Dybala amesema kuwa Cristiano Ronaldo ni mtu mgumu kuhusiana naye pale anaposhindwa kutimiza kile anachokitaka.

Dybala alifanyiwa mahojiano na Twitch, kujua uhusiano wake na Ronaldo na mipango yake mingine baada ya msimu huu.

Akizungumzia uhusiano wake na Ronaldo, Dybala alisema wakati wote yeye hutaka kushinda tu.

"Na mtu mgumu kuhusiana naye pale anaposhindwa kufikia malengo yake ya ushindi.

"Wote tunakaribia kufikisha mabao 100 na Juventus, nimebakiza bao moja yeye amebakiza matatu.

"Wakati wote hutaka kushinda, hata kwenye mazoezi pale anaposhindwa huwa ni kazi kushughulika naye kwa muda fulani, huwa anakasirika akishindwa."

Akizungumzia tetesi za Lionel Messi kutua hapo Juventus, Dybala amesema kuwa kulikuwa na ming'ono ya nyota huyo kuhamia Juve, lakini wao walidhani na waliona suala hilo ni gumu kutekelezeka, kwa sababu ni vigumu kuchagua kati ya Messi na Ronaldo.

## Bayern wapambana kumbakiza Flick



**BAYERN,** Ujerumani

MKURUGENZI Mtendaji wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge, amesema klabu hiyo inafanya kazi kwa karibu na Hansi Flick "kupata suluhisho" baada ya kocha huyo mkuu kutangaza nia yake ya kuondoka.

Flick alisema katika mahojiano na televisheni moja baada ya ushindi wa wiki iliyopita huko Wolfsburg kwamba, amewaomba 'wababe' hao wa Bavaria kufuta mkataba wake, ambao ulikuwa unafikia mwisho mwaka 2023.

Bodi ya Bayern Munich baadaye ilisema haijakubaliana na uamuzi wa Flick, wakati huu ambao mbio za kuwania taji la tisa la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, bado hazijafikia mwisho.

Lakini, wakati wa mazungumzo ya uwezekano wa kusimama kati ya pande hizo mbili, Rummenigge anamatumaini makubaliano yanaweza kufikiwa kabla ya mchezo ujao ambapo Bayern Munich watacheza dhidi ya Borussia Monchengladbach ifikapo Mei 8, mwaka huu.

Flick anahusishwa na mpango wa kuchukua mikoba ya kuinoa Timu ya Taifa ya Ujerumani, ambayo itakuwa wazi wakati bosi wa muda mrefu, Joachim Low atakapoondoka baada ya mashindano ya Euro 2020 mwaka huu.

## *Guardiola ampigia 'saluti' Sterling*

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola alisifia "kiwango cha kuvutia" kutoka kwa Raheem Sterling, licha ya fowadi huyo kuendelea kuwa na ukame wa mabao wakati Manchester City wakishinda taji la EFL, juzi Jumapili.

City ilishinda taji la EFL kwa mara ya nne mfululizo, huku mlinzi Aymeric Laporte ndiye akiibuka shujaa kwa kufunga bao pekee na la ushindi kwenye mchezo huo.

Sterling alipiga mashuti mara tano, lakini hakuweza kufunga na sasa hajafunga tangu alipofunga katika ushindi wa bao 1-0 wakati City ilipocheza dhidi ya Arsenal, Februari, mwaka huu.

Hata hivyo, winga huyo wa England alicheza kwa kiwango cha kuvutia mno akionana vizuri na Serge Aurier pamoja na Phil Foden.

Alipoulizwa kuhusu Sterling, Guardiola alisema mchezaji huyo wa zamani wa Liverpool amekuwa kwenye kiwango cha "kuvutia".


"Aliwaonyesha wapinzani wetu kwamba, tumekuja hapa kushinda mchezo tangu dakika ya kwanza. Alipambana kwa kadiri ya uwezo wake," alisema Guardiola mara baada ya mchezo huo.

Aidha Guardiola ana imani kwamba, Sterling atarudi kwenye uwezo wake wa kufunga hivi karibuni kwa kusema: "Hatuna shaka kuhusu hilo, kwani uwezo wake ni wa kiwango cha juu kabisa.

"Alitengeneza nafasi nyingi na kutoa pasi kadhaa kwa Ilkay (Gundogan). Wachezaji wote walikuwa kwenye kiwango bora."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN: NAJIVUNIA KUWA SEHEMU YA BARCA

Mfaransa huyo asema kwake ushindi wa timu ni muhimu zaidi na anafurahia kuona...

**BARCELONA,** Hispania

ANTOINE Griezmann anajisikia fahari kuwa sehemu ya Barcelona inayojiimarisha katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu, licha ya kuendelea kucheza nafasi tofauti.

**Mchezaji huyo wa Ufaransa alifunga mabao mawili wakati Barca ikiibuka na ushindi wa magoli 2-1 dhidi ya Villarreal Jumapili baada ya Samuel Chukwueze kuwaweka mbele wenyeji kwenye dimba la de la Ceramica.**

Sasa amefunga mabao 13 na kutoa pasi za mwisho tisa katika mashindano yote kwa kipindi cha mwaka 2021 - amepitwa na mchezaji mwenzake wa Barca, Lionel Messi (32) na nyota wa Villarreal, Gerard Moreno (24) ambao wamehusika na mabao mengi zaidi miongoni mwa wachezaji wa LaLiga.

Griezmann kwa mara nyingine alicheza kwa upatina mzuri na Messi kwenye mchezo huo dhidi ya Villarreal, huku Frenkie de Jong na Pedri walikuwa pamoja kwenye mfumo wa 3-5-2 ambao unapendwa zaidi na kocha, Ronald Koeman.

Wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kiutamaduni amekuwa akicheza zaidi kama mshambuliaji namba tisa wakati akiwa kule Atletico Madrid, ana furaha kuwa kwenye kikosi cha Barcelona kinachowania taji la LaLiga, licha ya kuchezeshwa nafasi tofauti.

"Najaribu kuwa pale, miongoni mwa washambuliaji wasaidizi," alisema akiiambia LaLiga TV.

"Nahitaji kutengeneza nguvu na kasi kwa wachezaji wenzangu ili wapate nafasi nzuri ya kufunga zaidi. "Sio nafasi yangu kiasili, lakini najivunia kuwa hapa Barcelona na kucheza na wachezaji wenzangu kama hawa.

"Mara zote nacheza kwa ajili ya ushindi wa timu, hivyo ninakuwa na furaha kubwa ninapoona naongoza kwenye ushindi kwa timu yetu"

Griezmann sasa amefunga katika mechi tatu mfululizo, na ushindi huo sasa umeifanya Barca kupunguza tofauti ya pointi na vinara Atletico kwa pointi mbili.

Barcelona sasa ipo nafasi ya tatu ikiwa na pointi 71 sawa na Real Madrid waliopo nafasi ya pili, huku Atletico wana pointi 73.

Hata hivyo, Barcelona wana mchezo mmoja mkononi.

## ZISIKUPITE

### VARANE ANUKIA CHELSEA

CHELSEA wapo mbele ya Manchester United na Paris St-Germain katika mbio za kutaka kumsajili beki wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Raphael Varane, 28. ***(Mundo Deportivo)***

### CAMARA AGOMBEWA EPL

BEKI wa Guinea, Ali Camara (23), ambaye anachezea klabu ya Young Boys ya ya Uswisi, amezivutia klabu kadhaa za Ligi Kuu England, zikiwamo Liverpool, Arsenal, Crystal Palace, West Ham United na Norwich. ***(Team Talk)***

### YAMTAKA NAGELSMAN

BAYERN Munich imeanza kufanya mazungumzo ya kutaka kumchukua kocha wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann. (***Independent)***

### WILLOCK HAKIJAELEWEKA

ARSENAL wapo njia panda juu ya mustakabali wa kiungo wao, Joe Willock, 21, ambaye yupo Newcastle kwa mkopo. Arsenal wanahitaji kuuza baadhi ya wachezaji ili kujiimarisha kifedha. ***(Football London)***

### AZPILICUETA SOKONI

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, ana nia ya kumsajili beki wa Timu ya Taifa Hispania, Cesar Azpilicueta, 31, kutoka Chelsea. ***(El Gol Digital)***

### BELOTTI AGOMBEWA

KLABU za Manchester United na Liverpool zinaweza kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Torino na Italia, Andrea Belotti, 27, ambaye pia anawaniwa na AC Milan, Roma na Inter. ***(Tuttosport)***

### ABRAHAM AGEUKA LULU

KLABU ya Wolverhampton Wanderers imeingia katika orodha ya timu zinazowania kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Tammy Abraham (23). Aston Villa, West Ham na Leicester City pia wanadaiwa kutaka kumsajili mshambuliaji huyo. ***(Football Insider)***

### KANE KUBAKIA SPURS

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Harry Redknapp, anategemea kuona mshambuliaji kinara, Harry Kane, 27, ataendelea kubakia katika klabu hiyo licha ya tetesi kwamba huenda akaondoka mwishoni mwa msimu.***(Goal)***

### CITY, BELGRADE ZATETA

MANCHESTER City wameanza majadiliano na Red Star Belgrade kwa nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wao kinda wa Serbia, Andrija Radulovic, 18. ***(Sun)***

### MORATA ANOGEWA JUVE

STRAIKA wa Hispania, Alvaro Morata mwenye umri wa miaka 28, amesema angependa kubakia Juventus ambako anacheza kwa mkopo akitokea Atletico Madrid. ***(Sky Italia via Goal)***

HABARI MICHEZO

# YANGA SC YAMPONGEZA DUBE KWA KUWAMALIZA

Na Saada Akida

KOCHA wa makipa wa Yanga, Razak Siwa, amemtetea golikipa wake, Faroukh Shikalo, kwa kuwa bao alilofungwa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga halitokani na uzembe bali ni uwezo binafsi na ujuzi wa mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube, ambaye alifunga goli hilo pekee katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi.

**Wakati Siwa akisema hayo, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati alisema kutoka kwa Carlos Carlihnos ilikuwa ni faida kubwa kwao kuongeza mashambulizi na hatimaye walifanikiwa kufunga bao pekee na la ushindi katika mchezo huo.**

Azam FC iliondoka na pointi tatu baada ya kupata ushindi wa bao 1-0, Dube akifunga bao hilo dakika ya 85 kwa shuti kali la nje ya 18 ambalo lilimshinda Shikalo kudaka.

Akizungumza na gazeti hili, Siwa alisema hawezi kumtupia lawama Shikalo kwa sababu mfungaji alitumia ufundi na ujuzi mkubwa wa kupiga mpira wa mbali na kuipa timu yake ushindi.

"Mpigaji alitumia ujuzi na alitumia akili ya kufunga, kufungwa haikuwa uzembe wa kipa wetu kwa sababu hata sisi tuliweza kupata nafasi waliyopata Azam FC kwa kupiga shuti la mbali na kushindwa kutumia vizuri nafasi,".

"Tulitengeneza nafasi nyingi hatukuweza kutumia kwa sababu hatukuwa watulivu ila wenzetu walipata walikuwa makini na utulivu mkubwa wa kupata ushindi huo," alisema Siwa.

Aliongeza baada ya matokeo mabaya waliyopata juzi, wanaenda kufanyia kazi upungufu wote uliojitokeza kwenye mechi hiyo kwa ajili ya kuwa imara kuelekea mchezo wao unaofuata wa Kombe la FA dhidi ya Tanzania Prisons ambao utachezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga.

Vivier alisema walikuwa na wakati mgumu sana kwao kucheza vizuri dhidi ya Yanga ambayo ilimwanzisha Carlihnos na hivyo walishindwa kupita katika mbinu zao.

"Kitendo cha kutolewa Carlihnos kwetu ilikuwa faida kubwa kwa sababu tuliweza kumzuia vizuri Mukoko Tonombe, alishindwa kuonekana na kwetu kupata nafasi ya kupata ushindi huu," alisema Vivier.

Kwa ushindi huo wa juzi usiku, Azam FC imefikisha pointi 54 na kuendelea kukaa katika nafasi ya tatu huku Yanga ikibaki ya pili na pointi 57 wakati mabingwa watetezi, Simba wanaoongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 58 lakini wamecheza mechi pungufu.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni, wakifanya mazoezi kwenye ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kujiandaa na fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (BSAFCON 2021), zinazotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu nchini Senegal. **PICHA: TFF**

## Straika Prisons aitamani Stars

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA tegemeo wa Tanzania Prisons, Jeremiah Juma, ambaye alifunga bao pekee katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ruvu Shooting iliyochezwa Jumapili iliyopita mjini Sumbawanga mkoani Rukwa, amesema lengo lake ni kurejea kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Aprili 18, mwaka huu mshambuliaji huyo pia alifunga mabao mawili katika ushindi wa magoli 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

Jeremiah alisema kukaa kwake muda mrefu bila kufunga mabao kulitokana na majeraha ya muda mrefu ambayo yalikuwa yamemwandama, lakini hata hivyo hivi sasa yuko fiti na ameanza kutupia.

Kwa sasa Jeremia ana mabao sita kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwa mmoja wa wachezaji wanaokiwania kiatu cha dhahabu, huku mabao yake yakiifanya Prisons kushika nafasi ya tisa, ikiwa na pointi 34, ikicheza michezo 26.

## Kijiji cha michezo Singida chanukia

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MAANDALIZI ya mradi wa ujenzi wa Kijiji cha Olimpiki unaoratibiwa na Olimpiki Afrika kupitia kwa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC) kitakachokuwa kikijihusisha na michezo mbalimbali yamekamilika, imeelezwa.

Taarifa hiyo imetolewa baada ya TOC kufanya ukaguzi na kuridhishwa na maendeleo ya kijiji hicho pamoja na hali ya hewa ya eneo lililotengwa kwa ajili ya mradi huo.

Ofisa Maendeleo ya Michezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Amani Mwaipaja alisema wamejipanga kuhakikisha wanamichezo kutoka kwenye halmashauri hiyo wanakuwa vinara kwenye michezo mbalimbali watakayoshindana.

Mwaipaja alisema anauhakika wanamichezo kutoka kwenye wilaya hiyo watapeperusha vyema bendera ya mkoa hasa katika upande wa mchezo wa riadha.

# *Dube akipotezea kiatu cha dhahabu Ligi Kuu Bara*

**Na Saada Akida**

WAKATI vita ya kuwania ufungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu imeendelea kupamba moto, mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube, amesema hafikirii tuzo hiyo na akili yake ameiweka katika kuisaidia klabu yake ifanye vyema.

Dube mwenye mabao 12 anaongoza katika msimamo wa wachezaji waliopachika mabao mengi akifuatiwa na mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Dube alisema malengo yake ni kuhakikisha kwanza anaona Azam FC inafanya vizuri katika mechi zote zilizosalia msimu huu halafu kuwania tuzo hiyo ya ufungaji bora yatafuata.

Alisema anaomba uzima na kuendelea kupata nafasi ya kucheza ndani ya kikosi cha timu hiyo ili kuendelea kuipambania timu yake na kutumia vyema nafasi anazopata ili kutimiza malengo yao.

"Kwanza tunahitaji kufanya vizuri kwenye michezo iliyobakia, kuhusu tuzo ya ufungaji bora nina imani muda utaongea kila kitu kitakuwa sawa," alisema Dube.


Wachezaji wengine wanaofuatia katika orodha ya wafungaji ni John Bocco wa Simba mwenye mabao 10, Fully Maganga (Ruvu Shooting), Ibrahim Meshack (Gwambina FC) na Daniel Lyanga (JKT Tanzania) ambayo wamecheka na nyavu mara nane huku waliofunga magoli saba ni pamoja na Clatous Chama (Simba), Ayoub Lyanga na Iddi Selemani 'Nado' (Azama FC), Yussuf Mhilu (Kagera Sugar) na Adam Adam (JKT Tanzania).

Wenye mabao sita ni Luis Miquissone na Chris Mugalu wa Simba, Deus Kaseke na Yacouba (Yanga) na Jeremiah Juma wa Tanzania Prisons.

# Michezo

Jumanne Aprili 27, 2021

Nipashe

‘Najivunia kuwa sehemu ya Barca’ UKURASA 22



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Saido Ntibazonkiza (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Azam FC, Nicholas Wadada katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. Yanga ilifungwa bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga, Azam FC zauota ubingwa

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya juzi kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Azam FC, nahodha wa Yanga, Haruna Niyonzima, amesema anaamini timu yao bado ina nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa mwaka 2020/21.

Wakati Niyonzima akisema hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin ‘Popat’ na nahodha wake, Aggrey Morris, wamesema wataendelea kupambana kwa mechi zilizosalia ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa kwa sababu bado mbio za kuwania taji hilo ziko wazi.

Niyonzima aliliambia gazeti hili kikosi chao kilicheza vizuri lakini kosa moja walilofanya liliwaruhusu Azam kulitumia vyema na kujipatia bao hilo la ushindi. Kiungo na nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Rwanda, aliwataka wachezaji wenzake kuendelea kushikamana katika kipindi hiki na wafahamu ni dhambi kukata tamaa.

“Kama hujafika mwisho wa kile unachopaswa kukifanya, hupaswi kukata tamaa,” alisema Niyonzima.

Popat alisema matokeo ya mechi ya mzunguko wa kwanza ambayo timu yake ilifungwa bao 1-0 yalimuumiza sana, lakini sasa maumivu yake yamekwisha.

“Wao walichukua tatu kwetu na sisi tumechukua kwao. Azam tulianza vizuri, tukatetereka na sasa tunamaliza vizuri. Tutapambana hadi dakika za mwisho kwa sababu bingwa bado hajatangazwa. Mwisho wa ligi ndiyo tutajua, lakini kwa sasa bado tunasaka ubingwa,” alisema Popat.

# Simba yaitisha Dodoma Jiji FC

## Yatamba itaendelea kutoa dozi huku wapinzani wao wakiahidi kuwapa ‘suprise’...

**Na Saada Akida**

TUMEREJEA! Baada ya kumaliza ratiba ya michezo yake katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, mabingwa watetezi, Simba wanatarajia kuwakaribisha Dodoma Jiji FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Ni mechi itakayowakutanisha mabingwa watupu kwa sababu Dodoma Jiji FC pia ndio mabingwa wa msimu uliopita wa Ligi Daraja la Kwanza, ambao waliwafunga Gwambina FC ya jijini Mwanza na kushinda taji hilo.**

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini jana kuelekea mchezo huo, makocha wa timu zote mbili kila mmoja amesema wanahitaji pointi tatu muhimu ili kuendelea kujiweka katika mazingira mazuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba iko kileleni ikiwa na pointi 58 lakini imecheza mechi pungufu tatu huku Dodoma Jiji FC yenye pointi 38 iko katika nafasi ya sita baada ya kushuka dimbani mara 27.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema baada ya kurejea jijini wakiwa na pointi tisa mkononi kutoka Kanda ya Ziwa, sasa wako tayari kwa ajili ya mchezo dhidi ya Dodoma jiji FC ambao pia wanahitaji kupata ushindi.

Matola alisema hesabu zao ni kutetea ubingwa wanaoushikilia na wanatambua Dodoma Jiji ni timu nzuri na wamejipanga kuingia uwanjani kupambana kwa sababu wanawaheshimu wapinzani wao huku wakikumbusha ushindani katika mechi iliyowakutanisha ya mzunguko wa kwanza.

“Mchezo huo tunauchukulia kwa uzito mkubwa na katika mechi yetu ya kesho (leo), tutakuwa na wachezaji wetu watatu ambao walikosa michezo iliyopita akiwamo Luis Miquissoine na Pascal Wawa, uwepo wao katika mechi hii utakiongezea nguvu kikosi chetu.”

“Tutaendelea kumkosa Taddeo Lwanga kutokana na kutokuwapo nchini, beki wetu alikwenda kwao kwa ajili ya matatizo ya kifamilia baada ya kufiwa na dada yake,” alisema Matola.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein ‘Zimbwe Jr’ alisema wamerudi kwenye uwanja wa nyumbani hivyo ana imani watapambana kuhakikisha wapata pointi tatu muhimu na kuendelea kujiimarisha kileleni.

“Tumerudi nyumbani na kucheza katika falsafa yetu ya kucheza soka, mashabiki wajitokeze kwa wingi ili kuendelea na kile ambacho tumekifanya Kanda ya Ziwa, sasa ni zamu ya Dodoma jiji FC,” alisema beki huyo ambaye anatajwa kuwaniwa na Yanga.

Naye Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji FC, Renatus Shija alisema wamejiandaa vizuri na wana ‘jambo lao’ dhidi ya Simba.

Shija alisema wamekuja kupambana na watahakikisha wanawastaajabisha wapinzani wao.

“Malengo yetu ni kupata pointi muhimu, tunajua Simba ni timu nzuri na wako bora ila kwa upande wetu tunaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo,” alisema Shija.

Mbwana Hamilton, nahodha wa Dodoma Jiji alisema wanawaheshimu Simba kwa sababu ni timu bora hapa nchini lakini wamejipanga pia kutumia udhaifu walionao katika kuwadhibiti.

“Ni mechi muhimu na kikubwa tutahakikisha tunafanya kazi tuliyotumwa, tumejiandaa kufanya vizuri katika michezo yote iliyobakia ikiwamo huu dhidi ya Simba ambao tutakutana nao kesho (leo),” alisema nahodha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >